# Nipashe

Jumamosi Juni 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579951

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Zitto ajitosa kupinga kodi ya taulo za kike


UKURASA 3




UKURASA 13

# Kipimo dengue kufanywa bure

UKURASA 2




Ummy Mwalimu

## Mbowe, wenzake wakwaa kisiki



UKURASA 3

## TISHIO LA UGAIDI: Jeshi lasambaza mashushushu

UKURASA 2

**MICHEZO** DA SILVA WA BRAZIL ASAINI MIWILI SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Kipimo cha dengue sasa bure

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAKATI ugonjwa wa homa ya dengue ukionekana kuwa tishio kila kona nchini, serikali imesema kuanzia sasa vipimo vya homa hiyo vitatolewa bure kwenye vituo vya afya vya umma wakati huu wa mlipuko.

Pamoja na uamuzi huo kupokewa kwa mikono mwili na wabunge, pia serikali imesema imeagiza mashine kubwa sita (fogging machine) kwa ajili ya kupulizia mbu wapevu ambazo zinatarajiwa kufika kabla ya mwishoni mwa Julai, mwaka huu.

Akiwasilisha kauli ya serikali bungeni jijini hapa jana kuhusu mlipuko wa homa ya dengue nchini, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema serikali imeamua vipimo hivyo vitolewe bure.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, wagonjwa 4,320 na vifo vinne vilivyotokana na homa ya dengue vimetolewa taarifa, huku mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi.

"Katika kuimarisha uchunguzi na matibabu ya homa ya dengue, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) imeshanunua vipimo 30,000 vya kupima ugonjwa huo," alisema.

Awali, Wizara ya Afya ilielekeza vituo vya umma vya kutolea huduma kutoa huduma ya vipimo vya dengue kwa utaratibu wa kawaida wa uchangiaji wa gharama za matibabu.

**HATUA ILIZOCHUKUA**

Alisema mpaka sasa serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuangamiza mazalia ya mbu wapevu na viluwiluwi na kwamba wizara imeishanunua lita 60,000 za viuavidudu kutoka kwenye kiwanda cha uzalishaji kilichoko Kibaha.

"Kati ya hizo lita 11,400 zimesambazwa kwenye halmashauri tano za mkoa wa Dar es Salaam, lita 48,600 zinazosambazwa kwenye halmashauri za mkoa wa Geita, lita 8,092, Kagera lita 12,308, Kigoma lita 7,616, Lindi lita 9,048 na Mtwara lita 11,536," alisema.

Waziri Ummy alisema lita zingine 36,000 zimeagizwa na zitasambazwa kwenye mikoa yenye mlipuko wa ugonjwa huo ikiwamo, Pwani, Morogoro, Tanga na Singida.

"Dawa za kunyunyuzia nje lita 2,000 kwa ajili ya kuua mbu wapevu pia zimeagizwa ambazo zitasambaza katika mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Tanga," alisema.

Alisema mpango mwingine ni kuunda kikosi kazi cha wataalamu cha kushughulikia udhibiti wa mbu wanaoeneza ugonjwa huo na malaria nchini na kikosi kazi hicho kitaimarisha jitihada za kudhibiti ndani ya Mikoa na Halmashauri zote nchini.

"Katika kuimarisha uchambuzi na matibabu ya ugonjwa wa homa ya dengue, bohari ya dawa imeshanunua vipimo 30,000 vya kupimia homa hiyo na awali Wizara ilielekeza vituo vya umma kutoa huduma ya vipimo kwa uchangiaji wa kawaida katika matibabu.

"Kutengeneza na kusambaza mwongozo wa matibabu ya ugonjwa huu kwa ajili ya watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma. Kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa nchi nzima kwa kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji wa taarifa na kwamba wizara

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kukutana na taasisi sita za wizara hiyo, ili kujipanga upya na kuboresha huduma wanazotoa. Kulia ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Ranchi ya Taifa (NARCO), Magembe Makoye na Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania, Prof. Faustin Lekule. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jeshi lasambaza mashushushu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amesema jeshi limesambaza maofisa wake kutoka idara ya intelijensia kutokana na kuwapo kwa taarifa za tishio la kufanyika kwa matukio ya kigaidi nchini.

Hata hivyo, IGP Sirro amesema taarifa walizonazo ni kwamba hadi sasa, Tanzania haina tishio la kufanyika kwa matukio ya kigaidi, lakini katika kuchukua tahadhari, tayari jeshi limeshapanga watu wake maeneo mbalimbali.

IGP Sirro alitoa kauli hiyo juzi baada ya Ubalozi wa Marekani nchini kutoa taarifa katika mtandao wake wa kijamii wa Twitter ukitahadharisha na kutoa angalizo la kiusalama ukidai kuna uwezekano wa kutokea shambulio la kigaidi katika baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam.

"Jeshi la Polisi tayari limepita kwenye hoteli mbalimbali na maeneo ya biashara na ili kuzungumza nao, tumepanga watu wetu maeneo mbalimbali, siwezi kuyasema, kuhakikisha kwamba kama likitaka kutokea, tutahakikisha tunalizuia, kama litatokea kwa bahati mbaya, tutahakikisha wahusika tunawapata.

Alisema Jeshi la Polisi huwa linapokea taarifa zote bila kujali ni ndogo kwa kiasi gani na kuzifanyika kazi.

Alisema taarifa ya Ubalozi wa Marekani ilitakiwa ipitie kwanza Jeshi la Polisi ili kuona ukweli wa jambo lenyewe kabla ya kutangazwa kwa umma.

"Kuna haya matishio ambayo toka tumeyapata si muda mrefu, lakini tumejipanga vizuri, niwahakikishie Watanzania tuna timu zetu za kutosha kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, tupo vizuri.

"Haya mambo mengine ambayo yameonekana kwenye mitandao, ni taarifa ambayo Jeshi la Polisi linazifanyia kazi, hata kama ni ndogo kiasi gani, tunazifanyia kazi," IPG Sirro alisema.

Aliongeza kuwa ndani ya jeshi hilo wapo wanaopata mafunzo kupitia ubalozi huo na wamepanga kuonana nao na kufanya mazungumzo ili waone taarifa iliyotolewa ikoje na kuifanyia kazi.

"Tanzania ipo vizuri sana, watu wetu wa intelijensia wapo vizuri, operesheni na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vipo vizuri, siku zote lazima tukae na tahadhari kwa sababu nchi yetu siyo kisiwa, ukiona inatokea nchi nyingine na kwetu inaweza kutokea, kikubwa ni ushirikiano, ukiona jambo halipo vizuri ambalo linatia shaka tupeni tuifanyie kazi," alisema.

Juzi, serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ulimwita Kaimu Balozi wa Marekani nchini ili kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa yao.

Mwaka 1998, ikiwa ni takriban miaka 21 sasa, wapiganaji wa Jihadi walishambulia kwa pamoja Balozi za Marekani za Kenya na Tanzania.

Agosti 7, mwaka huo, saa 4:30 asubuhi, wakati magaidi wawili walilipua lori moja lililokuwa limejaa mabomu mbele ya Ubalozi wa Marekani mjini Nairobi Kenya. Dakika tisa baadaye, bomu lingine lililipuka katika Ubalozi wa Marekani mjini Dar es Salaam.

Takriban watu 242 waliuawa katika mashambulizi hayo yalioharibu kwa kiwango kikubwa ofisi za balozi hizo za Marekani na kusababisha kuporomoka kwa nyumba zilizokuwa karibu.

## VAT yakwamisha ujenzi wa stendi mpya ya Dar

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, amesema ujenzi wa stendi mpya ya kisasa ya mabasi umekwama kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kuwa kubwa.

Amesema hali hiyo imesababisha vifaa walivyononunua kwa ajili ya kazi hiyo kukwama bandarini.

Liana aliyasema hayo jana mbele ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Sulemain Jafo, wakati akitoa maelezo ya mradi huo.

Jafo alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo pamoja na barabara zilizoko chini ya mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

"Serikali Kuu ilitupatia Sh. bilioni 50.95 bila VAT Januari 18, mwaka huu na mkandarasi alianza kazi na mpaka Juni 19, tumepata changamoto ya VAT. Nimekuwa nikifuatilia suala hilo hadi mkoani Dodoma pale Hazina, lakini mpaka sasa nimekwama," alisema.

Alisema wiki iliyopita alijulishwa kwamba kamati imeshakaa na kuidhinisha, hivyo kutokana na ucheleweshaji huo wana wasiwasi kwamba endapo mkandarasi ataruhusiwa kwenda kununua vitu, kuna uwezekano asirudishiwe fedha zake.

"Mheshimiwa Waziri tumesubiri sana tunaomba utusaidie tena katika suala hilo maana tumekwama na changamoto nyingine ilikuwa ya mvua kunyesha ilitusumbua sana, lakini hadi sasa tumefikia asilimia 20 ya kazi hii ya ujenzi. VAT ikishughulikiwa mapema itasaidia hata kumaliza kabla ya muda," alisema.

Waziri Jafo alisema tayari alishamweleza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kuhusiana na watu wake kukwama katika ujenzi kutokana na suala la VAT.

"Si kwamba mradi huu tu ndio umekwama. Miradi yote ya DMDP imekwama, nina imani kuwa Dk. Mpango atakwenda kulishughulikia kwani nilishamwambia na nimeandika barua kwa kuwa Rais (John Magufuli) ametoa fedha, hatuko tayari kuona unacheleweа huu mradi," alisema Jafo.

Aidha, Jafo alimtaka mkandarasi anayejenga mradi huo kuongeza kasi katika ujenzi huo na kwamba hataki kusikia kisingizio cha mvua

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Diwani Athuman, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa mradi wa maadili kupitia filamu ya bahasha. Kushoto ni Balozi wa Uholanzi hapa nchini, Florence Mattli. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Zitto ajitosa kupinga kodi ya taulo za kike

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), ameitaka serikali ijitafakari kama mwaka mmoja ilioutoa unatosha kupima matokeo ya sera ya mwaka jana iliyoruhusu msamaha wa kodi kwenye taulo za kike.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo amepinga pendekezo la serikali kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye taulo za kike, akiamini ni uamuzi wa haraka na unaharibu sifa ya Tanzania.

Zitto aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana, alipochangia mjadala kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/20 na mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika mapendekezo hayo ya bajeti ya Sh. trilioni 33.1, serikali imeweka wazi kuwa ina mpango wa kurejesha VAT kwenye taulo za kike iliyoifuta mwaka jana kwa kuwa uamuzi wake huo haukufanikiwa kupunguza bei ya bidhaa hiyo muhimu.

"Inawezekana kabisa serikali ikawa sawa, kwamba bei ya taulo za kike haikushuka kutokana na mapendekezo ambayo serikali iliyaleta, lakini serikali inapaswa itafakari, je, mwaka mmoja ambao utekelezaji umefanyika unatosha kuweza kupima matokeo ya sera ile ambayo iliyafanya mwaka jana?" Zitto alihoji.

"Ukurasa wa 38 wa hotuba ya Waziri wa Fedha (Dk. Philip Mpango), anasema pendekezo lile halijawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu na hasa kwa walengwa na badala yake pendekezo lile limefaidisha wafanyabiashara."

**INAENDELEA UK. 8**

## Bosi Tamwa atwaa tuzo uongozi bora

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, ametwaa tuzo ya 'Wanawake katika Uongozi' iliyotolewa na World Women Leaders Congress (WWLC).

Tuzo hizo zilitolewa Jumatano ya wiki hii jijini Dar es Saalam kwa wanawake viongozi wa Afrika Mashariki walioleta mabadiliko katika jamii, walioibua vipaji, wanawake mifano ya kuigwa na wenye uthubutu kutoka taasisi na mashirika mbalimbali ya binafsi na serikali kutoka katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Wanawake viongozi kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi walitunukiwa tuzo hizo kutokana na vigezo vya ushindi vilivyowekwa.

Akizungumzia tuzo hiyo, Rose alisema ni sehemu ya kuwatia moyo wanawake wengine kufanya bidii zaidi kwani kuna watu wanawakubali na wanaweza kuzitunuku kazi zao. "Wanawake wanaweza kuwa viongozi wazuri, tuzo hii inaeleza kuwa uongozi wa wanawake unakubalika, hii ni tuzo ya dunia, kumbe ulimwengu umekubali kuwa wanawake wanaweza kuwa viongozi," alisema Rose.

"Jamii kwa ujumla ikubali kuwa wanawake wanaweza kuwa viongozi. Wanahabari wafanye kazi zao kwa kujiamini, kazi zao zikajulikana na wasikatishwe tamaa na kitu chochote," alisema Rose.

Wengine waliotwaa tuzo hiyo kutoka Tanzania ni Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa Tanzania Women CEOs Roundtable, Emma Kawawa.

Tuzo hizo zinatolewa ili kuhamasisha wanawake viongozi katika sekta za umma na binafsi, kutambua mafanikio ya wanawake kikanda na kidunia pamoja na kuwatia moyo wanawake vijana kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

## Shauri kesi kina Mbowe latupwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Afrika Mashariki imetupilia mbali maombi ya dharura katika shauri namba mbili la mwaka 2019 lililofunguliwa na viongozi waandamizi wa vyama vya siasa vya upinzani nchini katika mahakama hiyo jijini Arusha.

Mahakama imechukua uamuzi huo baada ya upande wa walalamikaji kumwomba jaji anayesikiliza kesi hiyo, Monica Mungenyi, kusikiliza upande mmoja wa walalamikaji, kitendo kilichopingwa na mawakili wa serikali.

Baada ya kusikiliza shauri hilo kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa na upande wa waleta maombi, jopo la majaji liliamua kutupilia mbali shauri hilo kwa kile walichokieleza kuwa upande wa waleta maombi umeshindwa kuthibitisha kwa mahakama hiyo umuhimu wa kusikiliza shauri upande mmoja kwa kuwa masuala yaliyopo katika shauri hilo ni muhimu, hivyo ili haki itendeke ni vyema upande wa pili usikilizwe ndipo mahakama itoe uamuzi.

Kesi hiyo iliyosikilizwa na majaji watano wa mahakama hiyo; Monica Mugenyi, Faustine Ntezyilyayo, FakihiJundu, Audace Ngiye na Charles Nyachae, ilifunguliwa na viongozi wa vyama vya siasa wakiongozwa na Freeman Mbowe, Zitto Kabwe, Hashimu Rungwe, Seif Sharif Hamad na Salum Mwalim, wakipinga utekelezaji wa Sheria

**INAENDELEA UK. 8**


## ANATAFUTWA

**OSWARD EMANUEL NDELWA** anatafutwa na ndugu zake ana umri wa **miaka 42** alipotea **mwaka 1994** Desemba. Yoyote atakayemwona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0767 – 609680 au 0622 – 609680.**

Taarifa ya polisi: **MAB/RB/494/2019.**

***Zawadi nono itatolewa kwa atakayetoa taarifa za upatikanaji wake.***



115288602



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA WILAYA

KINONDONI

SHAURI LA MADAI NO 10 YA 2019

TUJIJENGE TANZANIA LIMITED ............................................MDAI

DHIDI YA

MOHAMED SULTAN HAMIMU T/A MARIANA INVESTMENT ..................... MDAIWA

JONAS LEONARD NDUNGURU T/A INVESTMENT.......................................MDAIWA

SALUMU ZAGA.......................................................................................MDAIWA

KWA.

MOHAMED SULTAN HAMIMU T/A MARIANA INVESTMENT
JONAS LEONARD NDUNGURU T/A INVESMENT
SALUMU ZAGA

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya madai yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi. Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **JUMATATU, Tarehe 24 Mwezi 06 Mwaka 2019 Saa 2:30 Asubuhi**

Kwa mujibu wa Madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima uleta hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **20 Mwezi 06 Mwaka 2019.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

215289102

# Raia Nigeria afungwa miaka 30 kwa kukutwa na dawa za kulevya

Na Hellen Mwango

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela raia wa Nigeria, Christian Ugbechi, baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha pipi 56 za dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride.

Aidha, mahakama hiyo imeagiza pipi alizokutwa nazo mtuhumiwa ziharibiwe kwa mujibu wa sheria.

Hukumu hiyo ilisomwa jana katika mahakama hiyo chini ya Jaji Sirrilius Matupa baada ya kusikiliza ushahidi wa watu 11 na vielelezo 22 kutoka upande wa Jamhuri dhidi ya mshtakiwa.

"Bila kuacha shaka, mahakama yangu baada ya kupitia ushahidi na vielelezo vya upande wa Jamhuri, imeridhika na ushahidi wa Jamhuri kweli alitenda kosa hilo na inamtia mshtakiwa hatiani," alisema Jaji Matupa.

Pia alisema kwa mujibu ya kifungu cha 15 kidogo cha (1) cha Sheria ya Udhibiti Dawa za Kulevya, mshtakiwa atakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 na pipi alizokutwa nazo ziliteketezwe kwa mujibu wa sheria.

Mapema Juni 19, mwaka huu, mshtakiwa alikutwa na hatia kabla ya kutolewa adhabu hiyo jana.

Hata hivyo, Jaji alisema pamoja na mshtakiwa kujitetea kwamba alifanyiwa upekuzi mara tatu na hakukutwa na kitu chochote, hivyo upande wa Jamhuri ulipaswa kuleta ushahidi wa CCTV, haikuwa lazima kuwapangia mashahidi wa kuwaleta na kwamba walikuwapo mashahidi wengine waliothibitisha mashtaka dhidi yake.

Alisema Mkemia Mkuu wa Serikali katika uchunguzi wake, amethibitisha dawa za kulevya alizo

INAENDELEA UK. 8

# Takukuru, Uswisi wanoa makamanda wa mashtaka

Na Romana Mallya

SERIKALI ya Uswis imetoa Dola 750,000 katika kuimarisha safu ya waendesha mashtaka ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Fedha hizo takribani Sh. bilioni 1.7, zimetumika katika programu ya kuwaongezea uwezo wa kiufundi watumishi wa Takukuru wa Idara ya Kuendesha Mashtaka.

Balozi wa Uswizi nchini, Florence Mattli, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano na wanahabari uliohusisha kuonyeshwa sinema ya Bahasha inayozungumzia rushwa.

Sinema hiyo ilizinduliwa tangu Julai mwaka jana kwenye tamasha la filamu la kimataifa la Zanzibar (ZIFF).

Aidha, alisema imetazamwa kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru, wakati watu wengine wameiona katika kumbi za sinema, kwenye DVD, mtandao wa kijamii na katika maonyesho yaliyofanyika Dar es Salaam na bungeni mwaka jana.

Balozi Mattli alisema serikali yake inashirikiana na vyombo vya habari na mashirika ya kiraia kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha za umma.

"Mapambano dhidi ya rushwa hufanikiwa ikiwa uongozi utakuwa na nia pamoja na uwezo wa kuyaendesha, lakini pia kwa kuungwa mkono na wadau wote katika jamii hii ni kazi ya taifa zima," alisema.

Aliwaambia wanahabari kuwa muda wake wa kukaa Tanzania

INAENDELEA UK. 5



Mafundi wa kampuni ya ukandarasi, wakiendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu katika Barabara ya Kituo cha Daladala cha Simu 2000, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Kizimbani kwa madai ya kutakatisha Dola 251,000

Na Hellen Mwango

MFANYABIASHARA Hamis Almas (51), amefikishwa mahakamani jijini Dar es Salaam, kujibu mashtaka ya uhujumu uchumi ukihusisha kutakatisha Dola za Marekani 251,600.

Almas alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salimu Ally, alikodaiwa kuwa alichukua fedha hizo akiahidi kusafirisha tani 6.8 za korosho. Wakili wa Serikali Wankyo Symon, alidai, kuwa kati ya Agosti 17 mwaka jana na Aprili 30 mwaka huu jijini Dar es Salaam mshtakiwa alitenda makosa hayo.

Ilidaiwa kuwa, Almas akiwa katika ofisi za Pride Come Limited, alijipatia Dola za Marekani 251,600 kutoka kwa Joan Blanch Domenech, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Spove Nuts.

Ilidaiwa, alijipatia fedha hizo akijaribu kudanganya kuwa Kampuni yake Pride Come Limited, ingesafirisha tani 6.8 za korosho kwenda nchini Hispania kwa niaba ya kampuni ya Spove Nuts wakati akijua si kweli.

Katika shitakà la pili, mshtakiwa huyo anadaiwa kutakatisha kiasi hicho cha fedha kwa kuzipokea kupitia akaunti yake iliyo katika benki ya Equity wakati akijua fedha hizo zimetokana na kosa la udanganyifu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, hakimu alimtaka mshtakiwa kutojibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi.

Upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuahirishwa hadi Julai 4, mwaka huu itakapotajwa na mshtakiwa alirudishwa rumande hadi tarehe hiyo.


## SUMAJKT AUCTION MART

## MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYO PEWA NA **TUJIJENGE TANZANIA LIMITED** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA ZIFUATAZO KAMA JEDWALI LINAVYOONESHA HAPA CHINI.

| no | JINA | MAHALIZILIPO | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SHINA REHEGE MWANUKE | MPAKANI KWEMBE | NYUMBA | 25/06/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 2 | REGINARD MIKE KIBULA /SAIDI KHAMIS NASORRO | MTONI KIJICHI-MBAGALA | NYUMBA | 06/07/2019 SAA 4:00 ASBH |
| 3 | PASCAL LINUS KIMOLO | MOGO- KIPAWA AREA ILA/KPW/MOG41/53 | NYUMBA | 29/06/2019 SAA 6:00 MCHN |

215289602

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14
2) Endapo Mteja atashindwa kumalizia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku 14 hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
3) Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.

**Kwa mawasiliano zaidi piga namba:- 0716004554 NA 0753063481**



## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALIILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Rose/Daniel Eliewaha Mshana | T 417 DHH Brevis | Makumbusho Yard | 06/07/2019 | RAISSA A/Mart |
| Saidi Idd Lipika | Nyumba yenye Hati | Kibaha -Mlandizi | 13/07/2019 | TAVIR A/Mart |
| Adam Marwa Mwita | Nyumba | Mwanamtoti – Kijichi mbagala | 06/07/2019 | Champion A/Mart |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**RAISA: 0652113262;**
**TAVIR Auctioneer:**
**CHAMPION Auctioneer:**

**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**
**0717495311/0718802350**
**0688056805/0742983700**

225289702

# HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza UK Aid. Wengine ni Mwanaharakati wa Haki za Watoto, Felistas Kalomo na Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anna Kulaya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## DC asimamisha ununuzi pamba karibu na jineri

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, ameagiza kufugwa kwa vituo vyote vinavyokusanya pamba karibu na ofisi za mashine za kuchambulia pamba (jineri) na kusitishwa kwa usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka kata moja kwenda nyingine wilayani hapa.

Amesema vituo hivyo vinapaswa kuwapo mita 500 mbali na ofisi za kampuni hizo ili kuepusha udanganyifu na ushawishi unaoweza kujitokeza baina ya wanunuzi wa pamba na vyama vya msingi vya ushirika (Amcos).

Kiswaga aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha robo ya tatu ya Baraza la Madiwani, kilichofanyika katika ukumbi wa Barideco mjini hapa.

Alisema ili kuweka takwimu sahihi za ununuzi wa pamba na utaratibu mzuri unaofuata miongozo na kanuni za Bodi ya Pamba, ni vyema vituo hivyo vikawa mbali mita 500 kufikia ofisi za kampuni za pamba.

Pia alisema ili kuwe na uendeshaji mzuri wa ununuzi wa pamba katika msimu huu, ni lazima kuwa na usimamizi wa kutosha kutoka kwa madiwani, watendaji wa kata na vijiji katika kuwabaini wanunuzi holela ambao wanawaibia wakulima na kukiuka utaratibu mzima uliowekwa na bodi.

Sambamba na hilo aliagiza mamlaka husika kuhakikisha zinasimamia usitishaji wa ununuzi wa pamba bila fedha ili kuepuka mgongano na misuguano ambayo inaweza kujitokeza baadaye.

Naye Diwani wa Nyakabindi, Elias Masanja, alisema mpaka sasa ununuzi wa pamba haujakaa vizuri na hali hiyo inaweza kusababisha halmashauri kushindwa kukusanya mapato ya ushuru wa zao hilo.

"Msimu wa ununuzi wa pamba toka utangazwe rasmi mpaka sasa haueleweki. Kampuni za pamba bado hazijaanza kununua pamba na wengi wao wamekuwa wakinunua pamba toka kwa wakulima bila kufuata utaratibu wa kupitia Amcos na hiyo itachangia halmashauri kukosa mapato," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Emmanuel Mgongo, aliahidi kusimamia ununuzi wa pamba ili kuhakikisha halmashauri yake inakusanya mapato stahiki kama walivyojiwekea malengo.

## Takukuru, Uswisi wanoa makamanda

**INATOKA UK. 4**

unakwisha na kuishukuru Takukuru kwa ushirikiano iliyompa kwa miaka minne.

"Jitihada za pamoja katika kupambana na rushwa zimezaa matunda na taasisi imepiga hatua kubwa katika uwezo wake kwenye idara ya mashtaka. Nina hakika kwamba chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu, Diwani Athumani, maendeleo haya na ushirikiano kati ya nchi zetu utaendelea kuwa wa mafanikio," alieleza.

Aidha, Mkurugenzi Athumani, alisema Takukuru, Balozi za Uswisi na Uholanzi kwa pamoja wanatekeleza mradi maalum wa kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa unaoitwa "Mradi wa Maadili" (Integrity Project), uliohusisha kutengeneza filamu ya Bahasha.

Mradi huo ulianza mwaka 2016, ukihusisha kuiandaa na kuirekodi kazi iliyofanyika jijini Arusha, kwa mujibu wa maelezo yake.

Alisema kuanzia Mei 6, mwaka huu, Takukuru, imefanya maonyesho ya sinema ya bahasha Wilaya ya Geita na Chato mkoani Geita, Muleba mkoani Kagera, Kahama, mkoani Shinyanga, Ilemela na Nyamagana jijini Mwanza na Arumeru na Arusha na kazi itaendelea hadi Oktoba 13, mwaka huu, wakati wa kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru.

Alisema licha ya filamu hiyo kuonyeshwa usiku, inakadiriwa wananchi zaidi ya 9,000 wameiona na kujifunza maudhui yake, kuuliza maswali na kujibiwa.

Athumani aliishukuru Serikali ya Uswiss kwa mchango mkubwa kwa Tanzania katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa.

## Wafanyakazi kuipaisha zaidi NMB

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Asasi za Fedha, Viwanda, Benki, Uzalishaji wa Nishati, Biashara na Kilimo (Fibuca), kimehimiza kuwapo mahusiano bora baina ya wafanyakazi na waajiri kwani ni msingi wa maendeleo na mafanikio ya uwekezaji.

Rais wa Fibuca, Joseph Massana, alisema hayo jana na kuongeza kuwa uhusiano ulioharibika lakini sasa umerejeshwa baina ya wafanyakazi na Benki ya NMB utaiwezesha taasisi hiyo kukua zaidi.

Massana alieleza hayo jana jijini Dar es Salaam mbele ya Kaimu Mkuu Idara ya Rasilimali Watu wa NMB, Emmanuel Akonaay, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa Fibuca kuhusu chama chao na majukumu yao.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Massana aliwaeleza washiriki hao wa mafunzo hayo ambao asilimia kubwa ni vijana kuwa moja ya jukumu lao ni kuisaidia benki kusonga mbele kimafanikio.

"Wakati wetu tuliipandisha kuanzia chini, tukainua hadi ilipo. Hatukuwa na nyongeza ya mshahara, malipo ya ziada, sare wala teknolojia iliyopo sasa. Lakini tuliiwezesha kupanda, matarajio yangu mtaipandisha zaidi," alisema Massana.

Rais wa Fibuca, aliwaeleza washiriki wa mafunzo hayo kuwa anategemea kupata maazimio kutoka kwao ambayo atayawasilisha NMB ili kutatua changamoto zilizopo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji NMB, Akonaay alisema uhusiano baina ya benki na Fibuca ulitetereka kidogo na kukiri kuwa mahusiano mazuri kati ya wafanyakazi na mwajiri huleta afya kwenye biashara.

"Chama cha wafanyakazi kipo kwa ajili ya kuwasilisha maslahi ya watumishi kwenda kwa mwajiri kwa ajili ya kuyatekeleza, hivyo kutokana na sintofahamu zilizotokea upande wa uongozi wa benki na chama mwaka jana kumesababisha kutetereka kidogo ingawa kwa sasa mahusiano yamerudi," alisema Akonaay.

Aidha, hali hiyo ilisababishwa mwajiri na wafanyakazi kutokaa meza moja kujadiliana mambo yatakayowezesha taasisi hiyo kuendelea, kwa mujibu wa maelezo yake.

"Tunaamini majadiliano kati ya mwajiri na wafanyakazi yatatazama uhalisia uliopo sasa, kwa sababu mteja ana machaguo mengi ya benki kwa sababu zipo zaidi ya 50.

Tena karibu zote zinatoa huduma zinazofanana tofauti na awali benki zilikuwa chache. "Kitakachotutofautisha na benki A, B au C ni huduma bora zitakazotolewa na kasi inayoendana na teknolojia, mafunzo na kuwajali wateja. Naamini mtajadili namna ya kuisaidia benki kukua na kuimarika zaidi," alisema kaimu mkuu huyo wa idara.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Stars fanyeni kweli kwa Senegal kesho

**BAADA** ya jana mashabiki wa soka kushuhudia fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zikifunguliwa kwa wenyeji, Misri kuvaana na Zimbabwe, kesho macho na masikio ya Watanzania yataelekezwa kwa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Taifa Stars itashuka dimbani kwenye fainali hizo ikiwa ni mara ya kwanza tangu mwaka 1980 iliposhiriki fainali hizo nchini Nigeria.

Katika mchezo wa kesho, Stars itaanza kutupa karata yake ya kwanza dhidi ya Senegal na kisha Alhamisi Juni 27 kurudi dimbani kuwavaa majirani zao, Kenya ('Harambee Stars') kabla ya Julai Mosi, mwaka huu kuhitimisha mechi zake za hatua ya makundi dhidi ya Algeria.

Mechi ya kesho ni ngumu sana kwa Stars kwani inakabiliana na timu inayoundwa na wachezaji wengi wenye vipaji na uwezo wa hali ya juu ukilinganisha na nyota hao wa Tanzania walioko chini ya Mnigeria Emmanuel Amunike.

Mbali na sifa hizo, lakini pia kikosi cha Senegal kina wachezaji wengi wenye uzoefu wa mechi za kimataifa na wanaocheza soka la kulipwa barani Ulaya, na pengine ahueni kwa Stars inaweza kuwa kukosekana kwa Sadio Mane aliyetoka kuipa Liverpool ubingwa wa Ulaya, ambaye atakuwa nje akitumikia adhabu ya kadi.

Kwa ujumla Mane ni mmoja tu kati ya wengi na huwezi kulinganisha nyota wa kikosi cha Senegal na Stars ambayo kwa asilimia kubwa inategemea uzoefu mkubwa kutoka kwa nahodha wake, Mbwana Samata anayecheza soka la kulipwa KRC Genk ya Ubelgiji.

Hata hivyo, Nipashe kama wadau wakubwa wa soka hapa nchini hatuna shaka wala hofu na Stars kwani tunaamini inaweza kuwashangaza wengi kutokana na dhamira ya wachezaji kutaka kuonyesha uwezo wao ili kujitafutia soko nje ya nchi.

Tunatambua Stars itaingia uwanjani kama timu ambayo haipewi nafasi ('underdog') na kama Senegal nayo itaidharau tunauhakika inaweza kuushangaza Ulimwengu.

Kama ambavyo Senegal iliweza kuishangaza dunia kwa kuwafunga mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia, Ufaransa kwenye fainali hizo zilizofanyika mwaka 2002 na kutinga robo fainali, ndivyo ambavyo Stars inaweza kufanya maajabu. Kinachotakiwa na ambacho Nipashe tunaamini benchi la ufundi la Stars litakifanyia au limeshakifanyia kazi nikuwajenga wachezaji kisaikolojia kwamba inawezekana.

Hilo litawasaidia wachezaji kuondoa woga na kujenga moyo wa upambanaji, lakini pia ni muhimu kuandaliwa kucheza kitimu zaidi kwani siku zote katika soka hiyo ndiyo silaha ya kukidhibiti kikosi kinachoundwa na nyota wengi.

Tunaamini hivyo kwani hata wakati Senegal inaichapa Ufaransa haikuwa na wachezaji wa kiwango cha juu wengi kama Mane, bali iliamini katika kucheza kitimu wakati huo Wafaransa wakiwa na nyota wa Kizazi cha Dhahabu kama Zinedine Zidane, Didier Deschamps, Thierry Henry na wengine. Kila mchezaji akitimiza jukumu lake ipasavyo, tunaamini inawezekana kabisa kwa Stars kupata matokeo kesho na kuishangaza dunia jambo ambalo litavutia mawakala wengi kumulika soka la Tanzania.

Wachezaji hawana budi kufahamu kwamba kushinda mechi ya kwanza kutawaongezea ari ya kuweza kufanya vizuri mechi zinazofuata na hatimaye kutinga robo fainali, hivyo kesho wanapaswa kucheza kufa au kupona.

Nipashe kama ilivyo kwa wadau wengine wa soka na Watanzania kwa ujumla tunaiombea Stars na tutaendelea kuitakia kila la kheri katika mechi zake zote kwenye michuano hiyo.




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Maneno ni kama fumo ...

**HUSEMWA** "Maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hayarudi." Maana yake neno analotamka mtu ni kama mkuki (fumo), likitoka halirudi na huweza kuleta madhara.

Twanasihiwa tuwe na tabia ya kuyatafakari maneno tuyasemayo. Ni vizuri kulipima neno kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye.

"Hadhari kabla ya hatari" maana yake ni vizuri kutahadhari kabla ya kufanya jambo tusije kufikwa na hatari au maangamizo. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na hadhari kabla ya kutenda mambo. Aidha, yatufunza tusiwe na tabia ya kudakia mambo bila ya tahadhari.

"Poteza" ni kitendo cha kusababisha kitu kuwa mahali kisipoonekana; sababisha kitu kipotee; pia tumia wakati vibaya. Hapa twapata potezana, potezea, potezeana, potezesha, potezewa na potezewa.

Gazeti fulani la michezo liliandika: "Kakolanya: Nitampoteza vibaya Manula." Kichwa cha habari hicho kilinishitua na kufanya nisome kwa makini ili nipate maana yake. Paragrafu ya nane kati ya 12 ndiyo iliyonivutia zaidi.

Aliongeza (Kakolanya): "Yanga nilikuwa namba moja, sikuwa napata ushindani, kitu ambacho kilinifanya nione nipo bora, kumbe nilijidanganya, lakini uwapo wa Manula Simba, utanifanya nipambane zaidi ili niwe bora zaidi na kumpora namba."

Ukurasa wa mbele wa gazeti hilo kuna picha ya Kakolanya akitia saini kuthibitisha sasa ni mchezaji halali wa Simba. Chini ya picha hiyo kuna maneno haya: "Kakolanya: Nitampoteza vibaya Manula."

Hapa ndipo paliponishitua. Mbona paragrafu zote 12 sikuona mstari wowote ulioandikwa Kakolanya kasema "Nitampoteza vibaya Manula?" Kama ndivyo, Kakolanya ana maana gani kusema "atampoteza vibaya Manula?" Maana ya 'poteza' ni kitendo cha kusababisha kitu kuwa mahali kisipoonekana. Maana ya 'vibaya' ni kisichokuwa katika hali nzuri.

Kama ni maneno ya mwandishi, yaweza kuleta chuki kati ya Kakolanya na Manula kila mmoja kudhani mwenziye ni mshirikina anayetaka kumnyang'anya tonge mdomoni!

Hata hivyo, katika paragrafu ya tisa Kakolanya alinukuliwa kusema: "Yanga nilikuwa namba moja, sikuwa napata ushindani, kitu ambacho kilinifanya nione niko bora, kumbe nilijidanganya, lakini uwapo wa Manula Simba utanifanya nipambane zaidi ili niwe bora zaidi na kumpora namba." Maneno ya "Nitampoteza vibaya Manula" yalitokea wapi?

"Hadhari kabla ya hatari." Ni vizuri kutahadhari kabla ya kufanya jambo tusije kufikwa na hatari au maangamizo. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na hadhari kabla ya kutenda mambo. Tusiwe na tabia ya kudakia mambo bila ya tahadhari. Tuandike maneno yanayotamkwa na msemaji bila kuongeza yetu au kutia chumvi. Ni kumtilia mdomoni maneno ambayo msemaji hakuyasema!

'Chama' ni neno lenye maana tatu lakini nitaeleza moja tu ambayo ni muungano wa watu wenye lengo moja. Kundi lenye kufuata kaida au silka fulani zenye kuegemea dini, siasa, misimamo ya jamii, uchumi, michezo au jambo lingine lolote lenye maazimio maalumu.

Kila mkoa nchini una vyama vinavyosimamia maendeleo ya mchezo wa kandanda, navyo vipo chini ya uangalizi wa Shirikisho la Vyama vya Kandanda nchini, TFF. Hata hivyo, shirikisho hilo limejikita zaidi kwenye klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara, hasa Simba na Yanga!

Jumamosi iliyopita, Yanga walikuwa na shughuli maalum iliyoitwa 'Kubwa Kuliko' (kuliko nini?) kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam. Lengo lilikuwa kupata shilingi bilioni 1.5 zitakazowasaidia kufanya usajili mzuri msimu ujao.

Kilichoshangaza wengi ni kutoonekana kiongozi yeyote wa juu wa TFF, ingawa walialikwa! Badala yake shirikisho hilo liliwakilishwa na Mwenyekiti wake wa Kamati ya Uchaguzi, Ally Mchungahela, jambo lililowahuzunisha wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga.

Yakatokea manung'uniko na malalamiko miongoni mwa waliokuwapo, wakisema hata Iftar iliyoandaliwa na klabu hiyo kwenye Hoteli ya Serena wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, viongozi wa TFF hawakuhudhuria, ingawa walialikwa! Kuna madai kuwa Simba ilipowaalika viongozi hao kushiriki Iftar walihudhuria.

Hali hii yaleta picha gani kwa wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga kuona baba mmoja (TFF) akiwabagua wanawe? Nadhani hii ndio sababu iliyomfanya Rais mstafu wa awamu ya nne, Jakaya Mrisho Kikwete kuwanasihi viongozi mbalimbali wa kandanda nchini kufanya uamuzi wa usawa bila kujali timu wanazozipenda.

Pia azivitaka klabu kubadilika ili kuwaendeleza vijana na kuwajenga wachezaji wa kigeni wasiokuwa na faida kwa Tanzania.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

# Bil.2.4/- zatumika kudhibiti mwendo magari

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MFUMO wa kuratibu mwenendo au kasi ya mabasi ya abiria nchini hadi sasa umeigharimu serikali Sh. bilioni 2.4, Bunge limeelezwa. Kazi ya ufungaji wa kifaa hicho kwenye mabasi inafanywa na kampuni ya Bsmart Technologies ya Malaysia, ikishirikiana na kampuni ya Computer Centre ya Tanzania.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema hayo jana bungeni mjini hapa kuwa fedha hizo zimetokana na mapato ya serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra).

Nditiye alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Cecilia Pareso, aliyetaka kujua mfumo wa 'Vehicle Tracking System' (VTS) umegharimu fedha kiasi gani, mzabuni wa kazi hiyo kwa nini hakupatikana kwa ushindani kwa kufuata sheria ya ununuzi na je, mfumo huo unaendeshwa kwa kusimamiwa na nani.

Mfumo huo wa VTS ni mfumo unaowezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za basi likiwa safarini ikiwa ni pamoja na kudhibiti ajali. Taarifa hizo ni pamoja na mwendokasi, mahali basi lilipo, matukio ya ajali na jina la dereva.

Kifaa hicho huchukua matukio na kuyarusha kupitia mfumo wa satelaiti na teknolojia ya 'Global Positioning System' (GPS) na kupitia mitandao ya simu yenye teknolojia za 'Global Packet Radio System' (GPRS).

"Mzabuni alipatikana kwa njia ya ushindani kwa mujibu wa kifungu cha 150 cha Kanuni ya Sheria ya Ununuzi Tangazo la Serikali namba 446 ya mwaka 2013. Zabuni hiyo ilitangazwa kupitia zabuni ya kimataifa namba EA/025/2015-2016/HQ/G/22 Januari 14, 2016, PPRA Tender Portal, Tanzania Procurement Journal, toleo namba ISS: 1821 VOL IX-No. 3, pia zabuni ilitangazwa kwenye tovuti ya Sumatra," alisema Nditiye.

Kuhusu usimamizi wa mfumo huo, Naibu Waziri Nditiye alisema mfumo huo unasimamiwa na kuendeshwa na Sumatra kupitia kituo maalum kilichoko Mikocheni, jijini Dar es Salaam.

Ili kuimarisha usimamizi wa mfumo huo, alisema Sumatra imeingia mkataba na kampuni ya Tera Technologies and Engineering kwa ajili ya kufunga vifaa hivyo kwenye magari.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Serikali yaridhia uboreshaji biashara

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BARAZA la Mawaziri, limeridhia kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa mazingira ya biashara nchini.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema bungeni jana kuwa serikali imeshaandaa mpango huo unaoitwa 'Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment for Tanzania'.

Alisema hayo wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rukia Kassim Ahmed, aliyeuliza kwa kuwa mazingira ya biashara nchini ni magumu kwa wafanyabiashara wa ndani na wa nje, ni lini serikali itaondoa urasimu ili wananchi wanufaike.

Ole Nasha alisema mpango wa utekelezaji umekamilika lakini pia tayari serikali imetekeleza baadhi ya mapendekezo ambayo ni ya kiutawala na yasiyohitaji mabadiliko ya sheria.

"Serikali imekuwa ikibuni na kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali kwa kuhakikisha uwapo wa mazingira bora ya ufanyaji wa biashara nchini. Kwa mwaka 2017, serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi ilifanya uchambuzi wa kina wa mazingira ya biashara nchini kwa sekta zote.

"Katika kufanya hivyo, serikali ilibaini changamoto mbalimbali zikiwamo mwingiliano wa sheria. Kutokana na changamoto hizo, serikali iliandaa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa mazingira ya biashara nchini ambao umeridhiwa na Baraza la Mawaziri kwa ajili ya utekelezaji," alisema Ole Nasha.

Alisema mfano katika sekta ya kilimo na mifugo, tozo 114 na tano za Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), zimeondolewa na mapendekezo ya kuondolewa tozo zingine kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 yamewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Kwa mujibu wa Ole Nasha, moja ya mafanikio ya jitihada zinazofanywa na serikali katika kuboresha mazingira ya biashara ni kwa Tanzania kuendelea kuongoza kwa uwezo wa kuvutia mitaji kutoka nje katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki tangu mwaka 2012.

Aidha, kwa mujibu wa ripoti ya uwekezaji ya dunia inayotolewa na Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD) ya mwaka 2018, Tanzania imeongoza katika nchi za Afrika ya Mashariki.

Tanzania imetajwa kuvutia mitaji yenye jumla ya Dola za Marekani 1,180 ikifuatiwa na Uganda kwa Dola 700.

# Madaktari kupangiwa kazi vituo vya serikali

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema madaktari wote waliosoma kwa fedha za serikali watapangwa katika vituo vya kazi na serikali.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Abdalah Chikota, Mbunge wa Nanyamba (CCM).

Katika swali lake la msingi, Chikota alitaka kujua mpango wa muda mfupi wa serikali wa kupeleka madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Ligula (Mtwara).

Alisema kwa sasa wako madaktari ambao wanasoma katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (Muhas) na mara watakapomaliza masomo yao watapangwa na serikali kule ambako kuna mahitaji ya madaktari hao.

Naibu Waziri alisema katika wakati huu wa mpito wakiwa wanasubiri kupeleka madaktari hao, serikali pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya NHIF wamekuwa wakiweka kambi mbalimbali wakiwa na madaktari bingwa ili kutoa huduma za kibingwa.

Akijibu swali la msingi la Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia, Dk. Ndugulile alisema wizara imefanya tathmini ya mahitaji ya madaktari bingwa na fani zao katika hospitali zote za mikoa, kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Alisema tathmini hiyo itawezesha utekelezaji wa uamuzi wa kuwapanga upya madaktari bingwa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya kila hospitali hizo.

"Lengo ni kuwa kila hospitali hizi zinakuwa na madaktari bingwa wa fani nane. Fani hizo ni pamoja na daktari bingwa magonjwa ya uzazi na wanawake, watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji, upasuaji wa mifupa, daktari wa huduma za dharura na magonjwa ya ajali," alisema.

Pia alisema madaktari wengine bingwa wanaohitajika katika hospitali hizo ni pamoja na wa huduma za usingizi na radiolojia.

# Kipimo cha dengue sasa bure

INATOKA UK. 2

inaendelea kupata taarifa za kila siku juu ya mwenendo wa ugonjwa huu na magonjwa mengine," alisema.

**MAAMBUKIZI YAPUNGUA**

Waziri Ummy alisema takwimu za hali ya ugonjwa huo zinaonyesha kuwa maambukizi mapya yameanza kupungua kutoka wagonjwa 2,494 kwa Mei, mwaka huu hadi wagonjwa 813 mwezi huu.

Pamoja na mambo mengine, Waziri huyo alisema changamoto ambazo wamekutana nazo katika kukabiliana na ugonjwa huo ni gharama za kupimia ugonjwa huo.

"Serikali kupitia Bohari ya Dawa imenunua vipimo moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji na hivyo kuviuza kwa bei nafuu ukilinganishwa gharama inayotozwa kutoka kwenye baadhi ya hospitali binafsi, bado wananchi wanashindwa kumudu gharama za uchangiaji matibabu ya ugonjwa huo," alisema. Alisema changamoto zingine ni ushirikishwaji wa jamii, pamoja na matibabu ya ugonjwa huo katika vituo vya kutolea huduma.

"Watoa huduma za afya kutokufuata kikamilifu miongozo ya matibabu ya ugonjwa wa homa ya dengue.

Alifafanua kuwa mkoa wa Dar es Salaam peke yake una wagonjwa 4,029 na vifo vitatu, Dodoma wagonjwa watatu na kifo kimoja, Tanga wagonjwa 207 kifo hakuna, Pwani 57 hakuna kifo, Morogoro 16 hakuna kifo, Arusha watatu hakuna kifo, Singida wawili hakuna kifo, na Kagera wawili hakuna kifo.

"Vifo vilivyotolewa taarifa ni kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, kimoja, Hindu Mandal kimoja na Hospitali ya Regency wawili."

## Shauri kesi kina Mbowe latupwa

INATOKA UK. 3

ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2019.

Kufuatia uamuzi huo, majaji waliutaka upande wa waleta maombi kupatia nakala ya maombi hayo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kujibu, na tarehe ya kusikiliza maombi hayo itapangwa baadaye.

Katika shauri hilo, upande wa serikali uliwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupitia Mawakili wa Serikali; Evarist Mashiba na Kombe wakati upande wa Mashtaka uliwakilishwana na Mawakili Fatma Karume, Jebra Kambole na John Malya.

## VAT yakwamisha ujenzi wa stendi

INATOKA UK. 2

kukwamisha ujenzi huo.

"Huu mradi mko nyuma kwa asilimia nane, sitaki kusikia mvua mkandarasi kama watu wanajenga baharini ambako kuna maji wewe uanshindwa nini hapa? Mbona baharini wanajenga?" Alihoji. "Hii miradi ni ya pekee na ndiyo maana Rais John Magufuli aliamua kutoa Sh. bilioni 268.75 haijawahi kutokea ni kwa mara ya kwanza zamani ilikuwa jiji linachukua mikopo kwa benki za kibiashara," alisema.

Alisema Rais Magufuli alitoa Sh. bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi huo wa kituo cha mabasi, hivyo ameridhishwa na utendaji kazi na kuwataka kukamilisha ndani ya muda.

Aidha, alimwagiza mshauri mwelekezi kuhakikisha anasimamia vizuri mradi huo na pasijitokeze kwa dosara ya aina yoyote.

"Ndiyo maana nilikuwa nakuuliza maswali mengi kuhusiana na huu mradi nataka kila kitu uwe unakijua wewe, mkandarasi anaweza kufanya vitu vidogo ili apate faida nataka mambo yaende vizuri hizi Sh. bilioni 50 ni nyingi," alisema.

Alisema stendi hiyo itakuwa kubwa na ya kisasa, hivyo ifikapo Septemba mwakani iwe imekamilika kabla ya kuelekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Mimi ninachotaka kabla ya kuingia katika Uchaguzi Mkuu tumuite Rais Magufuli kuja kufungua huu mradi lengo ni Watanzania waje kuona manufaa ya huu mradi," alisema Jafo.

Aidha, Jafo aliagiza kujengwa kwa haraka barabara ya Mbezi Makonde ambayo inaunganishwa na Old Bagamoyo kwani imekuwa ni kero kwa wananchi.

"Hii barabara hadi wataalamu wangu mmeisahau, mmepata tabu kufika nilikuwa nawaangalia tu kwa nini mmenipoteza kufika hapa. Wataalamu wangu msipojua hizo barabara hamuwezi kujua changamoto za wananchi wanazozipata," alisema Jafo.

## Zitto ajitosa kupinga kodi ya taulo za kike

INATOKA UK. 3

Alisema anaikumbusha serikali kwamba mwaka jana, ilitoa pendekezo la kuongeza kodi kwenye mafuta ghafi yanayotoka nje ya nchi ili kulinda wazalishaji wa mbegu za mafuta nchini, lakini uamuzi huo haujawa na matokeo chanya.

Zitto (pichani) alisema: "Nataka Bunge lako tukufu Mheshimiwa Naibu Spika, tutazame nini matokeo ya pendekezo lile ambalo serikali ililileta. Mwaka 2017, kabla ya kodi zile kupandishwa, tulikuwa tunalinda uzalishaji wa mazao ya mafuta.

"Tulikuwa tunazalisha tani milioni 6.6 mwaka 2017 kabla ya kupandisha kodi ili kudhibiti uagizaji wa mafuta kutoka nje, mwaka 2018, Mheshimiwa Naibu Spika, tumezalisha tani milioni 1.6.

"Yaani pendekezo ambalo serikali imelileta mwaka jana, matokeo yake hayakuzalisha tegemeo la uzalishaji wa mbegu kuongezeka," Zitto alisema na kuongeza kuwa anashangaa kuona serikali haijaja na pendekezo la kufuta pendekezo lake ambalo halijawa na matokeo mazuri.

Kwa kutumia mfano huo, Zitto alisema haiwezekani pendekezo la kikodi likazaa matunda ndani ya mwaka mmoja.

"Kodi imeanza Julai 2018, kuna watu walikuwa na bidhaa ambazo wamenunua hazikuwa na punguzo hilo, lazima watauza kwa bei ileile, pia fedha yetu imeporomoka thamani dhidi ya Dola ya Marekani na taulo hizi nyingi tunaagiza kutoka nje, je, tumetazama hili?"

"Serikali itazame vizuri na kutoa muda wa kutosha kama ilivyofanya katika mafuta. Mwaka jana, suala la taulo za kike tulikuwa mfano na India, Afrika Kusini na Australia, wametuiga?" Zitto alihoji.



Katika mjadala huo, Mbunge wa Bukoba Mjini, Willfred Lwakatare (Chadema), alimtaka Waziri Mpango, Dk. Philip Mpango kueleza ni maajabu atayaotumia kukusanya fedha zilizokadiriwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Aliliambia Bunge kuwa katika miaka yote ambayo amekuwa bungeni, hajawahi kuona wabunge wa CCM wanasema kuwa bajeti ni mbaya, bali wamekuwa wakisema ni ya wanyonge.

Mbunge huyo pia alihoji uwezo wa wataalamu wanaotengeneza bajeti nchini na kushauri wataalamu nchini wajaribu kufanya utafiti ili kubaini tatizo la msingi liliko.

"Tujaribu kuona kwanini miaka hadi miaka, tunatengeneza bajeti lakini haziondoi umasikini wa watu wetu. Tuna masikio, tuna macho, tunasikia, tunaona," Lwakatare alisema.

Lwakatare ambaye pia aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Usalama wa Chadema, alisema katika bajeti ya mwaka huu, Mamlaka ya Mapato (TRA) ilitembea na wawakilishi wa vyombo vya dola kwenda kudai fedha pamoja na kuanzisha vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, lakini imefanikiwa kukusanya wastani wa Sh. trilioni 1.2 kwa mwezi.

## Raia Nigeria afungwa miaka 30 kwa kukutwa na dawa za kulevya

INATOKA UK. 4

zichunguza ndizo alizokutwa nazo mshtakiwa huyo.

Kabla ya kusomwa kwa adhabu Jaji Matupa alitoa nafasi kwa Jamhuri kutoa hoja.

Wakili wa Serikali, Constantine Kakula, alidai kuwa hawana kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa, lakini aliiomba mahakama itoe adhabu kali iwe fundisho kwa watu wakiwamo raia wa nje wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Wakili wa utetezi, Jeremiah Ntobesya, aliomba mahakama kumpunguzia adhabu mteja wake kwa sababu ana mke na watoto wawili wanaomtegemea na pia mshtakiwa anasumbuliwa na matatizo ya moyo na kwamba amekaa gerezani kwa mwaka mmoja na nusu na kipindi hicho chote alikuwa na tabia njema.

Pia alisema, pamoja na kwamba kifungu cha sheria kinaamuru mshtakiwa kuhukumiwa kifungo cha maisha gerezani, lakini siyo lazima, itolewe adhabu hiyo, mahakama inaweza kuamua vinginevyo.

Mapema mahakamani hapo, katika ushahidi wake, askari wa upelelezi kutoka Kituo cha Uwanja wa Ndege, Konstebo Peter alidai kuwa aliandika maelezo ya mshtakiwa huyo na katika mahojiano alimweleza kuwa amemeza pipi za dawa za kulevya.

Alidai baada ya kueleza hayo alimweka mahabusu ili kuzitoa na kwamba hadi Januari 30, 2018 saa 10:30 jioni alitoa pipi 23 alizomeza.

Pia alidai walichukua kielelezo hicho na pipi zingine zilizokutwa kwenye begi na kuzipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo kwa pamoja zilikutwa na uzito wa gramu 947.17.

"Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa pipi zote zilikuwa ni dawa za kulevya ambazo ni Heroin Hydrochloride zilizochanganywa na Paracetamol Metronidazole na Papavirine," alidai Peter.

Mkuu wa Kituo cha Uwanja wa Ndege, Inspekta Dickson Haule, alidai siku ya tukio majira ya saa 8:00 mchana akiwa ofisini alijulishwa na askari huyo wa upelelezi kuwa kuna mtuhumiwa amekamatwa na dawa za kulevya.

Haule alidai baada ya taarifa hiyo alienda Ofisi ya Polisi Interpol walipokuwa na alishuhudia mtuhumiwa akipekuliwa ndipo aliona begi dogo la mgongoni kuna pipi 56 zikiwa zimeviringishwa ndani ya soksi mbili nyeusi.

Katika kesi hiyo, inadaiwa Januari 28, mwaka jana maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Ilala mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akisafirisha dawa hizo zenye uzito wa gramu 947.57.

# Waomba mifugo kuzuiwa kwenda Kenya

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa mifugo wilayani Longido mkoani hapa, wameiomba serikali kupiga marufuku mifugo kupelekwa katika soko la Kenya na badala yake watumie mnada wa Mivraf ulioko Kijiji cha Eworendeke, ili kuupa nguvu mnada huo.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa mnada huo, Dismas John, mkazi wa Dodoma ambaye pia ni mfanyabiashara wa mifugo, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kukamatwa na polisi wa Kenya wanapopeleka mifugo nchini humo.

Alisema wanalazimika kupeleka Kenya mifugo yao kwa sababu Wakenya hawataki kununua mifugo nchini bali wanataka wapelekewe kwao na sababu kubwa wanakwepa kodi ya Tanzania kuwa kubwa.

"Wenzetu wanaogopa kuja nchini kununua mifugo sababu kodi zetu ziko juu hasa ya uvushaji wa mifugo kwenda nje ya nchi. Tunavyowapelekea huko kutokana na kukosa msimamo wa serikali juu ya kuuza mifugo nje ya nchi, inatuletea shida hata sisi," alisema John.

Alisema katika usafirishaji huo wanapata usumbufu njiani wakati wa kupeleka ikiwamo kukamatwa na kuuza wakati mwingine kwa bei ndogo. "Kweli tunapata usumbufu njiani wakati wa kupeleka mifugo Kenya. Tunakamatwa na wakati mwingine tunauza mifugo kwa bei ya hasara, hivyo kuwapo kwa mnada wetu kijijini hapa kutatusaidia kutuepusha na adha yote hii," alisema.

Aidha, alisema kwa upande wa Kenya wamekuwa wakikataa kuingiza magari ya Tanzania yaliyobeba mifugo na kudai kuwa yatumike magari ya nchini mwao.

Kutokana na hali hiyo, alisema wafanyabiashara wanakandamizwa na kuwasababishia uchumi wao kuyumba.

"Hawaruhusu magari yetu ya Tanzania kuingia kwao. Tunapata gharama mara mbili juu ya usafiri, hatupati faida yoyote, hivyo kuepukana na haya yote bora kutumia mnada wetu," alisema.

Pia alisema kuwapo kwa mnada huo kutasaidia usalama wa mifugo yao pamoja na kupata wanunuzi na kuiomba serikali kuhakikisha kiwanda cha nyama kinachojengwa wilayani hapa kukamilika kwa wakati.

Akizindua mnada huo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliwataka wafanyabiashara hao kuacha tabia ya kutorosha mifugo kupeleka Kenya na endapo atabainika mtu yeyote anayefanya hivyo, atachukuliwa hatua za kisheria.



Mkuu Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza na wafanyabiashara wa Halmashauri ya Meru juzi, katika mkutano wa kusikiliza changamoto zinazowakabili. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# DC awatoa hofu wanaotaka kujiunga JKT

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewahakikishia mamia ya vijana waliojitokeza kutaka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwa usaili utafanyika kwa uwazi na ukweli.

Pia amesisitiza kuwa hakutakuwa na upendeleo zaidi ya kufuata sheria, sifa zinazotakiwa kwa vijana kujiunga na jeshi hilo.

Muro aliyasema hayo jana ofisini kwake wakati akizungumza na vijana waliojitokeza kuomba nafasi za kuingia katika mafunzo ya JKT.

Kwa sasa usaili wa kuandikisha vijana hao kwa Wilaya ya Arumeru unaendelea.

Alisema watahakikisha wanachagua vijana wote wenye sifa ya kujiunga na jeshi hilo na hawatamfumbia macho mtu yeyote ambaye atakuwa anawadanganya vijana hao, kuwa watoe fedha ndipo wapate nafasi.

"Wako watu wanaopita huko barabarani wakiomba fedha, huku wakiwa wanajinadi kwa kuwalaghai vijana hawa kuwa wana uwezo wakuwapa nafasi, kitu ambacho si kweli. Kuweni makini na msikubali kudanganywa mkatoa fedha zenu kwa sababu jambo hili tutafanya kwa uwazi na bila upendeleo wowote," alisema.

Alisisitiza kuwa atakayekamatwa anawalaghai vijana hao, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kuwaomba vijana hao kuwafichua watakaowafuata kuwarubuni.

Mkuu huyo wa wilaya pia alisema mara baada ya kukamilisha uchambuaji wa majina kwa vigezo vya sifa na nafasi zilizopo, watabandika majina kwa vijana watakaopita awamu ya kwanza na kisha kuingia awamu ya pili ya vipimo vya kubaini afya za vijana, kikiwamo kipimo cha dawa za kulevya.

Aliwapongeza vijana wote waliojitokeza kujiunga na JKT kwa sababu wameonyesha kwa vitendo kumuunga mkono Rais John Magufuli anayesisitiza kila mtu afanye kazi kwa weledi, ukweli na uaminifu.

"Vijana hawa wamejitokeza kwa wingi na hii wameonyesha dhamira nzuri ya kutaka kutumikia taifa lao kupitia ulinzi na usalama. nawapongeza sana kwani wameuonyesha uzalendo mzuri wa kutaka kutumikia taifa lao," alisema Muro.

Alisema wanaamini kuwa kunapokuwa na jeshi imara na jeshi lenye nidhamu, basi hilo ndilo jeshi sahihi kwa ajili ya kupambana, kulinda na kupigania taifa.

## EAC yakumbwa na uhaba wataalamu hifadhi jamii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NCHI za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati, bado zinakabiliwa na changamoto ya wataalamu katika sekta ya hifadhi ya jamii, hali inayochangiwa na kukosekana kwa vyuo vya kutosha vinavyotoa kozi za fani hiyo.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa imesababisha wengi kwenda kusoma nchi zingine na kwa gharama kubwa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbalo, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa chuo maalumu cha kutoa mafunzo ya elimu ya mifuko ya hifadhi ya jamii cha Afrika Mashariki na Kati, kinachosimamiwa na Jumuiya ya Mifuko ya Hifadhi Afrika Mashariki na Kati (ECASSA).

Alisema katika nchi hizo, bado kuna uhaba wa wataalamu waliobobea katika sekta hiyo, hivyo uwapo wa chuo hicho utasaidia kuondoa changamoto iliyokuwapo ya wataalamu kwenda kusoma, mbali na kuzalisha wataalamu wengi zaidi na kuziba pengo lililopo. "Wengi wanashindwa kwenda nje ya nchi kujiendeleza kutokana na gharama kuwa kubwa, hivyo uwapo wa chuo hiki utasaidia kuondoa changamoto ya ukosefu wa wataalamu waliobobea katika masuala ya hifadhi za jamii," alisema.

Dk. Ndumbalo alisema katika nchi za Afrika, bado asilimia ya watu wanaotumia huduma ya mifuko ya hifadhi ya jamii iko nyuma, hivyo elimu zaidi inatakiwa kutolewa ili watu wajue umuhimu wa kuitumia mifuko hiyo. Naye Naibu Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, Anthony Mavunde, alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na jumuiya hiyo katika kukuza uchumi, hivyo wataendelea kuwawezesha zaidi katika kufanikisha malengo yao waliyojiwekea.

Alisema uwapo wa chuo hicho utasaidia kupunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili katika sekta ya hifadhi ya jamii kwa kufanya utafiti mbalimbali utakaolenga kuleta maendeleo na kuinua uchumi wa nchi kwa ujumla. Katibu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Meshack Bandawe, alisema kwa muda mrefu jumuiya hiyo ilikuwa na ndoto ya kuanzisha chuo hicho kwa ajili ya sekta ya hifadhi ya jamii ambacho kitatoa wataalamu waliobobea na wa kutosha.

Alisema kupitia chuo hicho watatoa mafunzo ya kujiendeleza kwa watumishi wa mifuko hiyo, lengo likiwa ni kuendelea kuboresha sekta hiyo na kutoa huduma bora kwa wananchi wake.

# Mfumo hatarishi malezi ya watoto watajwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

IMEELEZWA kuwa mfumo wa malezi ya watoto wa umri wa miaka sifuri hadi sita, katika maeneo ya ujasiriamali yakiwamo sokoni, vituo vya mabasi, karakana za magari na nyumba za starehe una athari kubwa katika ukuaji wa ubongo wa mtoto.

Malezi hayo yamedaiwa kuwa yasipodhibitiwa yatachangia kwa asilimia kubwa kujenga taifa la kizazi kisicho na mwelekeo na kinachojihusisha na matukio ya uhalifu, dawa za kulevya na unywaji wa pombe uliokithiri na hatari kwa afya. Daktari bingwa mwandamizi wa afya ya jamii, uzazi na magonjwa ya wanawake, Dk. Moke Magoma, alisema hayo alipokuwa akizungumzia mfumo wa maisha hatarishi ya zaidi ya watoto 250 wanaolelewa ndani ya masoko ya Memorial, Soko Kuu, Mbuyuni, Pasua na Manyema katika Manispaa ya Moshi.

Dk. Magoma alisema hayo kutokana na utafiti uliofanywa na mradi wa kuongeza uelewa na uwajibikaji wa huduma bora za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (ECD), unatekelezwa na Muungano wa klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) kwa kushirikiana na Taasisi ya CiC ya Ireland.

"Ubongo wa mtoto huanza kujifunza vitu kuanzia miaka sifuri hadi sita. Leo unapomweka sokoni ambako kuna kelele, matusi, moshi, moto na mazingira mengine yasiyo salama ni kumwandaa kukua katika hali mbaya hapo baadaye na matokeo yake ni vigumu kutoa wataalamu kama daktari na mwanasheria," alisema.

Nao wafanyabiashara katika soko la Memorial, Esther Ramadhani, Salma Ngowi na Yasinta Mathias, walikiri watoto wao kulelewa katika mazingira ambayo ubongo wao huathirika kwa kutoshika masuala ya msingi bali malezi yasiyostahili.

"Hapa watoto tunawalea chini ya vibanda vyetu vya biashara. Tunajua akili zao zinaharibika, lakini hayo yote tunamwachai Mungu maana yeye ndiye anajua maisha tunayoishi huku. Utamuachia nani mtoto wakati hata fedha ya kula kuipata ni shida," alisema Ramadhani. Walikiri mara kadhaa watoto wanaokulia katika mazingira yasiyo rafiki hujifunza mambo yasiyoendana na umri wao, lakini pia huathiri akili pale wanapoanza shule za awali na msingi.

Wakizungumzia suala hilo, Mwenyeviti wa Soko la Memorial, Godfrey Shayo na mwenzake wa Mbuyuni, Lameck Mziray, walikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kuahidi kuweka mpango maalum wa utoaji wa elimu kuhusu athari za kuchanganya malezi ya watoto katika maeneo ya biashara.

"Hili suala la watoto kuwa na uwezekano mkubwa wa kuathirika kisaikolojia halina ubishi. Huku sokoni ni matusi tu, lugha chafu, jua kali na mvua. Lakini pia watoto hawana maeneo ya michezo unategemea ubongo wake utajifunza nini zaidi ya uhalifu na mambo yasiyoendana na umri wao?" Alihoji Shayo.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Walemavu), Stella Ikupa (kulia), akiteta jambo na Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi na Wasioona Taifa (Tasodeb), David Shaba, kwa kutumia lugha maalum ya 'palm hand writing', baada ya kuzindua mpango wa kuwezesha vijana wa Sense International Tanzania, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Dawa za minyoo zatolewa Siha

**Na Mary Mosha,** SIHA

SERIKALI imesema zimebaki siku chache za kutekelezwa kwa kampeni ya kitaifa ya utoaji wa dawa za vitamini A zinazozuia minyoo tumbo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro.

Hayo yalithibitishwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Valerian Juwal, na kwamba kampeni hiyo ilianza Juni Mosi na itamalizika Juni 30, mwaka huu.

"Ni kweli tumepokea maelekezo hayo, kimsingi kutakuwa na kutoa vitamini 'A' ya nyongeza ya unyweshaji dawa za minyoo tumbo katika wilaya yetu," alisema.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kampeni hiyo inafanyika kwa lengo la kudhibiti magonjwa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, Vitamini A ya nyongeza ya dawa na dawa za minyoo hutolewa kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 59 katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoko wilayani Siha.

Hospitali ya Wilaya ya Siha peke yake kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Andrew Method, inahudumia wakazi 116,313 (kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012) kutoka vijiji 60 vilivyoko kwenye Kata 17.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kama kituo cha afya baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani humo kutoa ekari 40 za ardhi.

# Aonya hatari kuibuka magonjwa ya mlipuko

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITi wa Taasisi ya Watumia Maji na Utunzaji Mazingira (Uwamasakwa), Frank Kimaro, amesema kuna uwezekano mkubwa wa kuibuka magonjwa ya mlipuko ikiwa wakulima hawatachukua hatua za haraka katika harakati za kujenga vyoo vya kisasa.

Kimaro alisema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa vijiji vya Cheki Maji, Kawaya na Mkarama vilivyoko wilayani Hai mkoani hapa, baada ya kutembelea mfereji wa kilimo cha umwagiliaji skimu ya Matambo na kukuta changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa vyoo katika maeneo hayo.

Alisema wakati umefika kwa wakulima kuanza kujenga vyoo vya kisasa bila kubweteka kwa kusubiria fedha kutoka serikalini kwa ajili ya kazi hiyo.

"Wakulima wa mpunga hamna budi kutumia sehemu ya fedha mnazopata kwenye mauzo kujenga vyoo ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko na hasa kipindupindu ambayo yanaweza kutokea kutokana na uchafu wa mazingira," alisema. "Baadhi ya wakulima wa mpunga wa maeneo haya hawana vyoo wengi wao wanajisaidia kwenye maji wanapokuwa katika mashamba hayo, hivyo kuwapo hatari ya kuibuka magonjwa ya mlipuko," aliongeza.

Mfereji wa Mtambo una matawi 11 ya umwagiliaji wa ekeri 300 na zaidi ya wakulima 5,000 wa vijiji vitatu wananufaika na kilimo hicho cha umwagiliaji cha mpunga na mboga.

Mwenyekiti wa Skimu hiyo, Kipingudu John, aliwataka wakulima wote ambao wamefanya mchepuo ambao si rasmi wafukie mara moja na wafanye utaratibu wa kuwaona viongozi ili kupata maji kwa njia halali na atakayekiuka utaratibu huo sheria itachukua mkondo wake.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkalama, Joseph Mzomo, alisema mwaka juzi serikali iliwataka wakulima hao kuchimba vyoo, lakini hadi leo amri hiyo haijatekelezwa na baadhi yao.





Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia), akibonyeza swichi ya umeme kuzindua umeme rasmi katika Shule ya Sekondari Bicha, Kata ya Kilimani, Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma juzi. Kushoto ni Diwani wa Kata hiyo, Bakari Kambi.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Taasisi yamkuna Waziri Mkuu

**Na Allan Isack,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa tuzo ya heshima kwa taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Pass kwa kuenzi mchango wake wa kuendeleza kilimo.

Pass imekuwa bega kwa bega kuwasaidia wakulima pamoja na serikali katika jitihada za kuikuza na kuiendeleza sekta ya kilimo.

Akizungumza wakati wa kongamano la kiuchumi lililofanyika jijini Dodoma, na kukutanisha mashirika na taasisi na binafsi zinazojihusisha na kilimo. Majaliwa alizipongeza taasisi na mashirika hayo, kwa kujitolea kuwasaidia wakulima kwa lengo la kuleta maendeleo.

"Tunawashukuru Pass kwa kuwa wadau wetu kwa kutoa huduma kwa wananchi kwa lengo la kuisaidia serikali kufika uchumi wa viwanda," alisema Majaliwa.

Majaliwa alisema, serikali imeweka nguvu katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha kilimo kinawanufaisha wakulima hususani maeneo ya vijijini kutokana na kilimo kuwa uti wa mgongo wa taifa letu.

Ofisa Mkuu Mwendeshaji wa taasisi hiyo, Anna Shanalingigwa, alisema tangu walipoanza kufanya kazi nchini, mwaka 2000, imetoa Sh. bilioni 712, kuwasaidia wajasiriamali wadogo wa kilimo 929,000, kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Pass imetoa huduma kwenye sekta mbalimbali kama mawasiliano na usafirishaji, ujenzi wa miundombinu, umwagiliaji na zana za kilimo.

"Tuna furaha sana kuona jitihada zetu zinatambuka siyo kwa wanufaika tu hata kwa serikali kutambua mchango wetu tunaoutoa kuwasaidia wanufaika," alisema Anna.

Mkurugenzi wa Pass, Nicomed Bohay, alisema kama nchi inataka kufikia malengo ya uchumi wa kati na wa viwanda ni lazima kutengeneza mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wadogo wa kilimo.

"Kama taasisi binafsi tuliowekeza maeneo mbalimbali sekta ya kilimo tumeshatekeleza , wajibu wetu na umuhimu wetu umeonekana kwa wajasiriamali kukuza na kuongeza biashara zao," alisema Bohay.

Aidha, alisema Pass imesaidia kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo kwa kuwapa mawazo yanayogeuzwa kuwa mtaji wa kufanya shughuli za kilimo kikiwamo cha mboga na matunda , pia ufugaji.

Alisema kwa mwaka 2019, wamepanga kutoa mafunzo kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo ambapo jumla ya familia 235, 253, zitanufaika na mafuzo hayo yanaweza kutengeneza ajira kwa watu 700,000, na yatagharimu fedha kiasi cha Sh. bilioni 210.6.

# Waipongeza NEC kuitii mahakama

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

KITUO cha Sheria na Haki za binadamu (LHRC) kimeipongeza Tume ya Uchaguzi (NEC), kukubaliana na uamuzi wa mahakama wa kuwaondoa wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi mkuu ujao.

LHRC, imeieleza hatua hiyo kuwa ni mwafaka na itasaidia kuufanya uchaguzi kuwa huru na wa haki.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Ana Henga, katika kongamano la kujadili mchakato wa rasimu ya katiba

mpya ilipo na inakoelekea.

Alisema katiba bora ni ile ambayo ina makubaliano ya wananchi, na ili kuipata ni lazima mwafaka ufikiwe na kila mmoja aridhie.

Alifafanua zaidi ya kuwa katiba iliyopo ina upungufu wa aina mbili ambao ni maudhui na mchakato ambao vitu hivyo vimebeba mambo mbalimbali.

Akifafanua kuhusiana na maudhui alisema kuna mambo ya haki za msingi ndani yake ambayo huwezi kwenda kudai mahakamani, ikiwamo elimu, afya, jambo ambalo wanahitaji kulijadili ili waweze kutoka na maazimio.

Alisema upungufu wa pili ni pamoja na katiba hiyo kuwa na mchanganyiko wa makundi maalumu ambayo ndani ya katiba hiyo hakuna ufafanuzi , likiwamo kundi la walemavu, wanawake, watoto pamoja na wakimbizi .

Aliongeza kuwa vyote hivyo vinahitaji kujadiliwa ili waweze kutoka na maazimio yanayokubalika na wengi.

"Hayo makundi ni ya muhimu sana lakini ndani ya katiba hiyo hayapo, kwa hiyo kama wadau tunahitaji kujadili na kutoa maazimio," alisema Henga.

Alisema kutokana na hayo ndiyo maana wamekutana ili kujadili na kutoka na maazimio ambayo yataleta tija kwa wananchi wote.

Wakili wa Kujitegemea Harold Sungusia, alisema mchakato ulioanza unaweza kusaidia kila mmoja kujua haki zake za msingi katika uchaguzi ujao, kutokana na ukweli kwamba wakurugenzi kwa sasa hawawezi kuusimamia.

Alisema changamoto iliyopo ni kubwa kwani ni jukumu la NEC kuchagua watu wa kusimamia uchaguzi ambao watasimamia kwa haki bila upendeleo.

Alisema miaka yote kumekuwa na malalamiko kuhusiana na uchaguzi, lakini ana imani kutokana na hili lililofanywa na mahakama la kutoa wakurugenzi kusimamia uchaguzi, malalamiko huenda yakapungua.

Alisema tume hiyo inapaswa kuwa na waajiriwa ambao itawatumia katika kusimamia uchaguzi ili kumaliza malalamiko yaliyojitokeza mara kwa mara.

# Tamisemi kuajiri wakaguzi 100

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imeomba kibali cha kuajiri wakaguzi wa ndani 100, watakaotumika katika ngazi za serikali za mitaa.

Naibu Waziri Josephat Kandege, alisema ofisi hiyo imewasilisha maombi ya kupata kibali cha ajira ya wakaguzi hao 100, ili kutatua changamoto ya uhaba wa watumishi wa kada hiyo katika sekretarieti za mikoa na serikali za mitaa.

Kandege aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa kazi wa wakaguzi wa ndani unaofanyika jijini Dodoma.

Aliwaambia wajumbe wakaguzi wa ndani ni watumishi muhimu na serikali, inawaamini na inatambua mchango wao katika usimamizi wa fedha na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Alisema ni vyema wakawepo kwenye ofisi hizo ili kazi hiyo ifanyike kwa ufanisi.

"Napenda mfahamu kuwa watumishi hawa ndilo jicho la kwanza la serikali bila ninyi serikali haiwezi kuona vitu ambavyo vinatokea kwenye matumizi ya fedha, mmekuwa mkituonyesha yale yote yanayotendeka kinyume na matumizi stahiki yaliyoelekezwa..."

Akizungumzia changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa vitengo vya ukaguzi alisema serikali imeongeza bajeti za vitengo vya ukaguzi kutokaa Sh. bilioni 5.6 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia bilioni 6.4 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 14.3.

Wakati huo huo, Kandege aliagiza vitengo vya ukaguzi wa ndani kuhakikisha mianya yote ya ubadhirifu inabainishwa na kudhibitiwa kwenye mifumo ya kukusanyia mapato na usimamizi wa fedha.

Pia aliziagiza halmashauri zote kuhakikisha hoja zote za Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Fedha za Serikali (CAG) zinapatiwa majibu.

Aidha, kuhakikiwa na kufungwa, ushirikiano unatolewa kwa CAG na taratibu za kufunga hoja zinazingatiwa.


Aidha, Kandege, alimpongeza aliyekuwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali Mohamed Mtonga, kwa kustaafu utumishi wa umma na kazi kubwa aliyoifanya katika kada hiyo ya ukaguzi.

Akizungumza wakati wa mkutano huo Katibu Mkuu Tamisemi, Joseph Nyamhanga, alisema kutokana na umuhimu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani fedha zilizotengwa kwenye bajeti zitalindwa na kuhakikisha zinatumika kwa ajili ya kazi za kitengo pekee.

"Umefika muda sasa vitengo vya wakaguzi wa ndani kuimarishwa na kila mkoa na halmashauri kuviwezesha vitengo hivi kwa fedha, watu na vitendea kazi vya kutosha wakati wote," alisema Nyamhanga.

Aidha, Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi na Ufuatiliaji Ofisi ya Rais Tamisemi, Miriam Mbanga, alisema mkutano wa kazi kwa wakaguzi wa ndani wa mikoa na halmashauri ni wa kwanza kufanyika na unalenga kujifunza zaidi.

Aliongeza kuwa pia umekusudia kubadilishana uzoefu, kushirikishana namna mbalimbali ya kutatua changamoto za kiukaguzi na kujiwekea malengo ya namna ya kufanya kazi ya ukaguzi wa ufanisi.





# Waahidi kutoongeza kodi mwaka huu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) haitaongeza kiwango cha kodi kwa wafanyabiashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Akiwasilisha bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali, Waziri wa Fedha, Balozi Muhammed Ramia, alisema kuwa mpango huo wa kutopandisha kodi, utawanufaisha wananchi na wafanyabiashara.

Alisema kuwa serikali inakusudia kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayokusanywa ili kuziba mianya inayosababisha upotevu.

Alisema hatua hiyo haitoathiri mabadiliko ya kodi za Serikali za Muungano zilizopendekezwa katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Akizungumzia kuhusu mishahara ya wafanyakazi alisema serikali inatarajia kufanya marekebisho kwa wafanyakazi wenye uzoefu ili kuimarisha maslahi ya watumishi hao.

Alisema marekebisho hayo hayatawahusu wafanyakazi wote bali ni kwa wale walioutumikia miaka mingi ambao nyongeza zao zimetolewa kwa awamu mbili tofauti.

Alizungumzia deni la taifa, akisema limeongezeka na kufikia asilimia 57 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 800 kutoka Sh. bilioni 137.5

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kutumia jumla ya Sh. trilioni 1.4 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Balozi Ramia alisema kati ya fedha hizo mapato ya ndani ni Sh. bilioni 976.5 na ruzuku ya mikopo kutoka nje ni Sh. bilioni 394.6, ambapo ruzuku ya Sh. bilioni 8.3 ni mfuko wa wafadhili na Sh. bilioni 40 ni mikopo ya ndani.

Aidha, alisema kuwa misamaha ya kodi imekuwa ikipoteza mapato ya serikali hasa pale inapotumiwa vibaya.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020 serikali itazifanyia mapitio kanuni za vigezo vya misamaha ya kodi zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar, ili ziweze kuendana na hali halisi ya mahitaji ya misamaha hiyo, pamoja na kuziba mianya iliyojitokeza katika usimamizi.

Alisema ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, serikali inakusudia kuangalia uwezekano wa kutumia miongozo ya Umoja wa Mataifa (UN), katika utoaji wa misamaha kwa miradi ya maendeleo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akimwapisha Meja Said Ali Juma Shamuhuna kuwa Mkuu wa Kikosi cha Valantia Zanzibar, Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wanawake waelezwa mbinu kumiliki ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kufuata taratibu zilizowekwa na serikali wanaponunua viwanja, mashamba au nyumba ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Wito huo ulitolewa na Ofisa wa Ardhi, Haji Mrisho, alipokuwa akitoa elimu kwa wananchi wa Shehia za Mahonda na Tunguu kwa nyakati tofauti kuhusiana na umiliki wa ardhi hasa kwa wanawake.

Alisema kuwa kumiliki ardhi ni haki ya kila mtu awe mwanamke au mwanamume, lakini kuna taratibu zake ambazo ukizifuata hautakutana na tatizo lolote.

Alieleza kwamba migogoro mingi ambayo imekuwa ikitokea mara kwa mara inasababishwa na watu kutofuata taratibu wakati wakufanya manunuzi.

"Kuna taratibu kuu za kufuata ili mtu aweze kupata ardhi iwe kutoka kwa serikali, kununua kwa mujibu wa sheria, utambuzi, kurithi, hiba na kiwanja," alisema.

Alisema ni wajibu wa kila mmoja kuzifuata taratibu hizo kwani kufanya hivyo unaifanya sehemu yako uliyoinunua kuwa salama na kutokuwa na migogoro.

"Linapojitokeza suala la ardhi tusipuuze ni lazima tufuate taratibu za kiserikali ili ardhi zetu ziwe salama," alisema.

Akizungumza katika mikutano hiyo Katibu wa Mtandao wa Ardhi wa Wanawake Wilaya ya Kati Unguja, Bahati Issa, alisema kuwa mtandao wao umeibuliwa ili kumtetea mwanamke kutokana na kile ambacho kinaonekana kuwa ni kuonekana kama hana haki ya kukimiliki.

"Tunachokitaka ni wanawake kumiliki ardhi na msidhani kama kudhalilishwa ni kubakwa tu bali hata kunyang'anywa ardhi pia ni udhalilishaji," alisema Issa.

Kwa upande wake Msaidizi wa Sheria kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) Ofisi za Zanzibar, Fatma Kwale, alisema lengo la kutoa elimu hiyo kwa wanawake ni kutaka kujua ni vipi wanawake wanamiliki ardhi na uelewa wao juu ya suala hilo.

Aidha, Issa alisema kuwa Tamwa kwa kushirikiana na Shirika la Foundation for Civil Society, imetoa elimu kwa wananchi hususan wanawake ambao bado wana uwelewa mdogo juu ya rasilimali hiyo.

Alieleza kuwa ardhi ni rasilimali muhimu ambayo kila mmoja anatakiwa kuwa na umiliki ambao utaratibu wake wa kusajili na kutafuta hatimiliki ni wa msingi ili kuwa mmiliki halali.

Aidha, hatua hiyo ni muhimu ili isionekane kama ni wanaume pekee ndiyo wenye uwezo huo.

# Wataka wanaokosea kimaadili wasaidiwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAULI ya Mwakilishi wa Jimbo la Chaani Nadir Abdulatif, aliyetaka watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja (mashoga) kutoajiriwa na serikali, na walipo kufukuzwa kazi imezusha mijadala tofauti, visiwani Zanzibar.

Akizungumza na wanahabari Mwenyekiti wa Kamati ya Kupinga Vitendo vya Udhalilishaji wa Kijinsia, Nassor Hamad Omar, alisema:

"Kauli iliyotolewa na mwakilishi huyo ndani ya Baraza la Wawakilishi ni ya kibaguzi ikiwa na lengo la kuwavunja moyo vijana wa aina hiyo ambao wengine tayari wamefanikiwa kurekebisha tabia zao."

Alisema vijana wanaofanya vitendo vya mapenzi ya jinsia moja hawakupenda kuwa hivyo, lakini hayo ni matokeo ya ushawishi kutoka kwa jamii ambayo ni sehemu ya ukatili wa kijinsia.

Alisema wameanza harakati za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia tangu mwaka 2013 kupitia Jumuiya ya Maimamu Zanzibar na kuyakabili makundi hayo ambapo mafanikio makubwa yamepatikana.

Aliyataja mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na baadhi ya vijana waliokuwa wakijishughulisha na vitendo hivyo kuacha na kurudi katika jamii ya familia zao kama zamani.

''Kauli za kutowaajiri serikalini au kuwafukuza kazi si nzuri kwani huko ni sawa na kuwavunja moyo au kuwatenga katika jamii," alisema.

Aliongeza kuwa watafanya ushawishi wa kurekebisha tabia zao na kurudi katika familia na jamii kama zamani.

Mmoja ya kijana ambaye alikuwa akifanya vitendo vya ushoga na sasa, ameachana navyo, na kurudi katika jamii, (jina tunalo) alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, kwa juhudi zake za makusudi za kusambaratisha makundi hayo kuachana na vitendo hivyo.

Alisema nasaha pamoja na ushawishi huo kwa kiasi kikubwa umesaidia kujenga imani na kuweza kuacha vitendo hivyo na sasa kukubalika katika jamii, huku wengine wakiajiriwa katika sekta mbalimbali.

''Kinachoharibika hakitupwi, hutengenezwa na sisi tulikuwa tumejiingiza katika vitendo ambavyo havikubaliki katika jamii si kwa hiari yetu na sasa tumerudi katika jamii,'' alisema kijana huyo.

Alisema ni vyema kudhibiti waharibifu wanaowaharibu vijana na watoto, akidai wengine ni viongozi wakuu serikalini ili lengo liweze kufanikiwa na si kuwahujumu peke yao mashoga.

Hivi karibuni akichangia bajeti ya Wizara ya Afya, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatif, alitaka watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja wasiajiriwe katika utumishi wa umma kutokana na mienendo isiyo kubalika.



Soma UK. 14
Posh


Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI JUNI 22, 2019



# AIBU YAKE
## Mastaa wamshukia TID

UK.15

## BASI SAWA



# Cheed afurahia sauti yake

MWANAMUZIKI kutoka kundi la King Music, Cheed, alisema sauti yake nyembamba imemfanya kupendwa na kuwa kitambulisho chake.
Akizungumza hivi karibuni, Cheed alisema wako walioifananisha sauti yake na jinsia ya kike, lakini kwake imekuwa ni jambo la furaha kutokana na kupata mashabiki wengi wanaovutiwa naye.
"Wanamuziki wengi wana kitu ambacho kinawatofautisha na wengine, wako wanaosema sauti yangu inafanana na ya kike, lakini kwangu naona ni jambo la furaha kutokana na wengi wanapoisikia wanakuwa na hamu ya kuniona," amesema Cheed.



# Sholo akubali 'Ndembe Remix' shida tupu

BAADA ya kutoa singo yao kali 'Ndembe Remix', mwanamuziki wa miondoko ya Singeli, Sholo Mwamba, amesema ilikuwa kazi ngumu kuchanganya sauti ya muziki huo na ule wa Hip hop.
Katika kibao hicho wanamuziki wengine walioshiriki ni B Gway, G Nako na Mesen Selekta.
"Ndembe Remix umeleta mapinduzi katika tasnia ya muziki kutokana na kuchanganya ladha mbili ambazo watu hawakuzoea. Mimi nilipoambiwa niingize sauti nilipata wakati mgumu lakini hatimaye nilifanikiwa kwa kiasi kikubwa," amesema Sholo.



# Posh Queen habari nyingine

MREMBO na mwanamitindo Jacqueline Obed maarufu kama 'Posh Queen' ameibua hekaheka katika maeneo ya jengo la Bunge baada ya kwenda hapo kuangalia shughuli zinazofanywa na watunga sheria.
Moja ya picha zilizosambaa kwa kasi ni ile ya Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule 'Prof Jay' ambayo imepostiwa katika mtandao wa Instagram ambayo ilionekana wawili hao wameshikana mikono.
Mashabiki na watu mbalimbali wameonekana kuvutiwa na picha hiyo huku wengine wakienda mbali kuzungumzia umbo la mwanadada huyo ambaye amekatika kisawasawa.

## INSTA-TWITTER





**Imebaki** siku moja tu Taif Stars icheze mechi yake ya kwanza ya michuano ya AFCON 2019 dhidi ya Senegal. Nakwambia uzalendo kwanza ni lazima kuishangilia timu yetu ya taifa - **Hamisa Mobeto.**



**Hautafanikiwa** kama unafanya mambo hayo hayo kila siku - **Madee Ali.**



## Idris ebu kuwa na huruma na X-wako Wema

MCHEKESHAJI wa Tanzania, Idriss Sultan amewataka watu wanaojaza mitandao kwa kumpa pole msanii wa filamu, Wema Sepetu, kwenda gerezani kumjulia hali.

Wema amerudishwa mahabusu baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuamuru kwenda ndani kwa muda wa siku 7 kutokana na kukiuka hati ya dhamana.

Idris amewahoji wadau kuwa wanahisi maaskari wanamwonyesha hizo pole akiwa huko mahabusu? Huku akisema kuwa hizo pole zitamsaidia zaidi zikimfikia mwenyewe.




@burudanitele

>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**



# AIBU YAKE
# Mastaa wamshukia TID

SAKATA la kupigwa kwa msanii wa muziki wa Bongofleva, Khalid Mohamed 'TID', limechukua sura mpya baada ya baadhi ya mastaa kumshambulia wakidai ana tabia isiyovumilika.

Majuzi mwanamuziki huyo aliibua taharuki mitandaoni baada ya kuposti picha ikimwonyesha akiwa na majeraha usoni na kudai kashambuliwa na majambazi.

Hata hivyo, haikuchukua muda ilitoka video fupi ambayo alionekana TID akipigana baada ya kutokea mabishano na jamaa mmoja.

Mcheza filamu maarufu, Kulwa Kikumba maarufu 'Dude' ameingilia sakata hilo kwa kumshambulia TID akisema amejishushia hadhi kwa kitendo chake cha kupigana hadharani na kurusha picha ya aina hiyo mtandaoni.

"TID ni mwanamuziki mkubwa hakupaswa kupigana hadharani, hii ni tabia isiyovumilika na inaleta taswira mbaya kwa wasanii," amesema Dude.

Ameeleza kwamba tukio hilo si la kwanza kumuhusisha mwanamuziki huyo, kwani miaka ya nyuma alifungwa jela kwa kupigana.


"Imefikia wakati anatakiwa kujitambua yeye ni nani katika jamii, matendo yake yatamfanya kuheshimika au kudharauliwa na watu," ameongeza. Hata hivyo mwenyewe anakana kuanzisha ugomvi huo, badala yake amemtupia lawama jamaa huyo akieleza alikuwa akimfuatilia kila siku hasa baada ya kuona ameanza kupata mafanikio katika kazi zake.

## INSTA-TWITTER

Tuffollow/ Tu-tag
@burudanitele



**Sio** kwamba hatucheki kwa sababu tumezeeka 'nop' tunazeeka kwa sababu hatujawahi kucheka -**Billnass.**



**Nasikia** urafiki wao hawa umekwisha kabisa. Zimebaki salamu za juu juu. Team Wema mlimdai sana Sh. milioni 13 zenu. Nadhani aliweka kinyongo. Chuki na kinyongo ni uchafu wa moyo, ni hasara kuwa nayo -**Maimatha Jesse.**



**Watafiti** wanasema Wahaya na Waluguru wote wanapenda sifa ila zinatofautiana, wenzetu wao sifa za kisomi na siye Waluguru za kawaida tu, hii ni kweli au msemo tu? - **Babu Tale.**

# Kuumbe!

# 'USIKU WA MSWAHILI'

## TAMASHA PEKEE LA TAARABU LINALOCHANGIA ELIMU



TAMASHA kubwa la burudani lilopewa jina la Usiku wa 'Mswahili' linatarajiwa kufanyika mwaka huu likiwa na sura mpya.

Kulingana na waandaji wake Manispaa ya Ilala, tamasha hilo ambalo lilifanyika kwa mara ya kwanza miaka miwili iliyopita lina lengo la kuwakutanisha wazazi, walezi na wadau mbalimbali kuchangia maendeleo ya elimu ya msingi.

Akizungumza na BT, Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Ilala, Elizabeth Thomas, amesema mwaka huu tamasha hilo linakuwa na utofauti kimtazamo na wasanii watakaotoa burudani.

Amsema lengo la kuandaa burudani hiyo ni kuchangia ununuzi wa madawati kwa shule za msingi katika halamashauri hiyo.

Katika mwonekano huo mpya, tamasha hilo linatarajiwa kufanyika katika ukumbi mkubwa wenye kutosha watu wengi na kuwashirikisha wasanii wakubwa wa muziki wa taarabu na muziki wenye maadhi ya pwani.

"Mwaka juzi tulifanya tamasha katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Tambaza, safari hii tunatarajia kupata ukumbi mkubwa kama Diamond Jubelee ili wazazi na wadau kuingia kwa wingi," amesema Elizabeth.

Amsema katika utaratibu huo mpya wasanii wakubwa wataalikwa kutumbuiza pamoja na kupata nafasi ya kukutana na wazazi na wadau kujadili namna ya kukuza elimu ndani ya Manispaa hiyo.

Katika tamasha lilopita magwiji wa taarab nchini walioshiriki ni bendi ya Gusa Gusa Min Band, Old Is Gold na Mohd Ilyas,

Wengine ni Malkia wa mipasho nchini, Khadija Kopa, Isha Mashauzi na Khadija Yusuph.

Aidha, Elizabeth amesema mipango itakapokamilika utaratibu wa kupata tiketi utawekwa wazi kwa kila mkazi wa jiji la Dar es Salaam anayeguswa na elimu aweze kupata kwa urahisi.



DC Ilala Sophia Mjema

# WAMEFARIKI JUNI KAMA MICHAEL JACKSON

**Na Adam Fungamwango**

JUMATANO ijayo ambayo itakuwa Juni 25, dunia itakuwa kwenye kumbukumbu ya miaka 10 ya mwanamuziki maarufu kuwahi kutokea Michael Jackson, aliyefariki mwaka 2009 huko California nchini Marekani.

Katika kumbukumbu hiyo, hapa nchini Tanzania tutawakumbuka wanamuziki wa dansi waliofariki mwezi kama huu kwenye miaka tofauti.

Wakati nchini Marekani wataukumbuka mwezi Juni kuwa ndiyo aliofariki staa wao huyo, nchini Tanzania tutawakumbuka baadhi ya wanamuziki maarufu kabisa nchini ambao nao walifariki mwezi kama huo na kuacha majonzi makubwa kwa familia zao, pamoja na mashabiki wa muziki wa dansi nchini.



**Abel Bathazar 6 JUNI 1994**

Juni 6, mwaka 1994, alifariki mwanamuziki maarufu na mpiga gita ongozi la solo, Abel Bathazar.

Ni miaka 25 sasa tangu atutoke, akiwa kwenye bendi ya Magereza. nyimbo yake ya mwisho maarufu kupiga solo ilikuwa ni 'Ashura' ulioimbwa na mwimbaji wa kike, Nana Njige ambaye naye ni marehemu.

Akitokea Kilosa, alijiunga na NUTA Jazz na kupiga karibuni nyimbo zote za bendi hiyo kwa mtindo wa Msondo Ngoma hadi alipohama mwaka 1977 kwenda kuunda bendi ya Dar International.

Mwaka mmoja baadaye akiwa na kundi la Dar International na baadhi ya Msondo waliunda kundi la Mlimani Park Orchestra. Mbali na muziki alijaliwa ushawishi mkubwa kwa wanamuziki na ndiyo maana alikuwa na uwezo wa kuwazoa na kuwapeleka kuunda bendi nyingine, mfano mwaka 1985 alipowazoa wanamuziki wa Sikinde na kwenda kuunda Orchetra Safari Sound (OSS) kwa mtindowa Ndekule.

**Suleiman Mbwembwe 12, Juni 2004**

Ni miaka 15 sasa imetimu tangu tasnia ya muziki ilipompoteza mwimbaji wa sauti ya kwanza kali nchini Suleiman Mbwembwe. Wakati anafariki alikuwa kwenye kundi la Msondo Ngoma Music Band.

Alipotia bendi mbalimbali ikiwemo Tanzania Stars na wimbo uliomtoa ni 'Vicky', ambao uliwafanya Msondo kumchukua. Huko akiungana na kina TX Moshi walifanya mambo makubwa, yeye akitunga nyimbo kama 'Mtoto Nampenda', 'Kaka Nassor', 'Kaka Shaaban', 'Prisila' na nyinginezo. Hiyo ilikuwa ni katikati ya miaka ya '80. Mwanzoni na miaka ya '90 alijiunga na Vijana Jazz na kuimba na kutunga nyimbo nyingi ikiwamo 'Mama Chichi'.

Alirejea Msondo mwanzoni mwa miaka ya 2000, na kutunga nyimbo kama 'Mzee wa Miba' na nyinginezo. Alifariki mwezi kama huu terehe 12, mwaka 2004.

**Athumani Momba 18, Juni 2005**

Mwaka mmoja baada ya kifo cha Mbwembwe, tena ikiwa mwezi Juni, siku sita tu baada ya kuadhimisha mwaka mmoja wa kifo chake, alifariki mwanamuziki mwingine wa Msondo, Athumani Momba. Aliacha kibao chake maarufu alichomtungia mkewe 'Lucy Bandawe'. Momba aliyefariki Juni 18, 2005 , alianza kujulikana alipokuwa na bendi ya Vijana Jazz mwanzoni mwa miaka ya '80 kwenye kibao cha 'Maisha ya Amba'. Kabla ya hapo alikuwa kwenye bendi ya Dar International.

Muda mfupi baadaye aliondoka Vijana na kujiunga na Bima Lee ambako aliimba sauti ya kwanza kwenye karibuni nyimbo zote akishirikiana na Shaaban Dede.

Alichukuliwa na Msondo mwaka 1990, lakini baadaye alirejea tena Vijana, kabla ya kurejeshwa tena Msondo ambako alihudumu hadi alipofariki dunia. Kwa sasa ni miaka 14 tangu alipotutoka.

**Harila Tongolanga 4 Juni 2017**

Huyu ni mtunzi na mwimbaji maarufu zaidi wa nyimbo za Kimakonde. Alianza kujulikana mwishoni mwa miaka ya '80 alipotoa kibao cha 'Kila Munu Ave na Kwao' akiwa na CTU Les Mwenge ya Arusha.

Baadaye alianzisha bendi ya Makondeko Six band ambayo ilitamba na nyimbo kama 'Kila Munu Ave na Kwao' ikiwa na sehemu ya pili hadi ya nne, 'Saidaru', na nyingine nyingi. Harila pia alikuwa na kundi la zing zong la Bana Mwambe akiwa na akina Tx Moshi, lakini pia akiwa na mialiko mingi nchini Msumbiji. Alifariki dunia Juni 17 kwenye Hospitali ya Muhimbili alipokuwa amelazwa, kwa sasa ni miaka miwili tangu atutoke.

**Shaaban Dede- 6 Juni 2017**

Siku mbili baadaye baada ya kufo cha Tongolanga, mwanamuziki mwingine maarufu nchini alifariki dunia kwenye Hospitali hiyo hiyo ya Muhimbili. Wanamuziki walikuwa wakienda kuwaangalia wagonjwa wote wawili. Lakini kwa bahati mbaya wote walifariki kwa siku mbili tofauti. Dede ambaye naye alifariki mwezi kama huu, tarehe 6 Juni 2017, ni mtunzi, mwimbaji wa sauti ya kwanza na ndiye aliyekuwa akiziba pengo la Hassan Rehani Bitchuka kila alikokwenda.

Ni mmoja wa wanamuziki waliopigia bendi nyingi nchini kama Juwata Jazz, DDC Mlimani Park, OSS, Bima Lee, huku nyingine akizirudia kujiunga mara mbilimbili. Alifariki akiwa kwenye bendi ya Msondo Ngoma. Baadhi ya nyimbo zake alizotunga akiwa na bendi mbalimbali ni 'Jefa', 'Talaka Rejea', 'Shangwe ya Harusi,' 'Pole Mzee' na nyingine nyingi.

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0682 808 694**



# Mke mpya wa kukata tamaa Damu isiyopotea

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii inaitwa 'Mke Mpya wa Kukata tamaa'. Imechezwa na baadhi ya wasanii nguli akiwamo Nassor Awadh maarufu kama 'Chekibudi', pia Shamsa Ford.

Ni filamu ambayo ukiiangalia inafundisha vitu vingi, ikiwamo kuwa na huruma, lakini pia mara nyingi wenye kutenda mema hulipwa maovu.

Vile vile inaonyesha kuwa damu ya mtu huwa haipotei. Shamsa anafanya kazi ya mama lishe na ana msichana wake wa kazi ambaye anamsaidia kusambaza chakula.

Hata hivyo kadri zinavyozidi kusonga mbele hali ya msichana huyo inakuwa mbaya. Tayari alishakuwa mjamzito. Taarifa zikafika kwao. Msichana huyo alikuwa akiishi kwa baba yake mdogo ambaye ni Chekibudi.

Chekibudi baada ya kusikia mtoto wa kaka yake ni mjamzito aliamua kumfukuza nyumbani hapo kwa kumtupia vitu vyake nje.

Msichana huyo ilibidi akajisitiri kwa bosi wake Shamsa. Hata hivyo kitendo cha kuishi naye mle ndani kilimkera mume wa Shamsa, hivyo badala ya kuendelea na ugomvi na mumewe akaamua kumpa nauli ili akamtafute aliyempa ujauzito.

Akapanda basi hadi jijini Dar es Salaam na alipofika na kuulizia, aliambiwa huko nako alishaondoka.

Alikata tamaa na kuamua kutafuta kazi ya muda mfupi ili kumwezesha kuishi mjini hapo. Siku zilipotimua alijifungua mtoto wake ana kumuita Nando.

Hata hivyo, mama huyo hakuishi kwa muda mrefu akafariki dunia na kumuacha mtoto wake Nando.

Alipotimua umri wa miaka 17 aligundua sehemu ambayo mama yake alificha barua aliyoiandika kuhusu ukweli wa mambo yote yale.

Ndipo alipogundua kuwa mama yake alifariki kwa ugonjwa wa ukimwi, baba yake ni nani na mimba ile aliipatia wapi na akitaka kutafuta ukweli wa yote aanzie wapi.


Nando anaamua kufunga safari kwenda moja kwa moja hadi Kigoma alikotoka mama yake na katika kufuata ramani, alifika kwenye mgahawa ambao mama yake aliandika kuwa ndiyo alikuwa akiufanyia kazi.

Baada ya kujitambulisha na kuongea maneno machache, Shamsa aligundua kuwa yule alikuwa ni mtoto wa msichana wake wa kazi aliyeondoka miaka mingi iliyopita kutokana na kupata ujauzito.

Anaamua kumpeleka ilipo nyumba ya mama yake mkubwa ambaye alishakuwa mwendawazimu, huku baba yake mkubwa akiwa ameshafariki dunia.

Kama vile haitoshi, Nando bado anaulizia majirani baba yake ni nani, na hatimaye anampata baba yake mzazi.

Baba naye anasema aliamua kuikataa mimba kutokana na mambo mabaya aliyofanyiwa na mama yake Nando. Lakini yote yakawa yamepita, kijana akawa ameshampata baba yake mzazi.




# MIPASHO TU!

## CHRIS AMSHAMBULIA KARRUNCHE

Ni mwendo wa mipasho tu! Ndiyo hali halisi ya kupeana vijembe na mipasho inayowazunguka kila siku wasanii maarufu Rapper Chris Brown na mpenzi wake wa zamani Karrunche Tran.

Brown na Karrunche licha ya kuachana, lakini bado wanafuatana kila kona na kusababisha kila mara kupararuana kuwa kupeana vijembe.

Kitendo cha wiki iliyopita kwa Chriss kupayuka mtandaoni akimshambulia mchumba mpya wa mrembo huyo aitwaye Victor Cruz, kwamba hajui kuvaa ni mwendelezo wawili hao kutafutana.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, mwanamuziki huyo maarufu wa Marekani amemshauri mrembo Karrueche ampeleka kwake mwanaume wake ili amfundishe kuvaa vizuri.

Tukio hilo, limejiri baada ya Karrueche kuposti picha akiwa na Vicror kisha Chris Brown akaanza kutoa maneno hayo kwenye kisanduku cha maoni.

Wiki iliyopita ilikuwa ni wiki ya wanaume kupendeza, hivyo Karrueche na mpenzi wake huyo waliposti picha kwenye mitandao ya kijamii ambazo zilikuwa zinawaonesha wakiwa mitaani mjini Miami.

Kwenye maoni hayo yamesomeka "Sio kwamba ni wivu, ila jitahidi kumvalisha. Anaonekana kama nguo zilizowekwa kwenye kinyago na mnunuzi anataka kupunguziwa bei".

Chris Brown alishawahi kuwa kwenye mahusiano na Karrueche na tangu waachane Chris amekuwa akimfuatilia kwa ukaribu kwenye mitandao ya kijamii.

# Koffi Olomide na kifo cha mende



KASHFA za ubakaji bado zinamwandama mwanamuziki wa Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo Koffi Olomide, baada ya matamasha yake ya Afrika Kusini kufutwa kutokana na kupatikana na hatia ya kumbaka mnenguaji wake.

Kwa mujibu wa BBC, Olomide, mwenye umri wa miaka 62, ambaye jina lake halisi ni Antoine Agbepa Mumba, alitazamiwa kucheza muziki wake katika ukumbi wa Gallagher Convention Centre uliopo nje ya mji wa Johannesburg Juni 28 na Shimmy Beach Club mjini Cape Town siku mbili baadaye.

Lakini amepata upinzani kwenye mitandao ya kijamii na hatimaye matamasha hayo kufutiliwa mbali.

"Tafadhari mnafahamishwa onyesho la Koffi Olomide halitafanyika," alieleza mkurugenzi mkuu wa Convention Centre, Charles Wilson.



## We Hushpippi kuwakoga wenzio kwa noti ndiyo nini?

KATIKA kuonyesha jeuri ya fedha, supastaa Hushpuppi amevunja rekodi baada ya kuamua kukodi ndege binafsi ya kumsafirisha kutoka Ufaransa hadi Nigeria.

Hushpuppi ambaye anatamba kwenye mitandao, alitumia kiasi cha naira milioni 25.2 kukodi ndege hiyo baada ya ile ya awali kumuacha.

Kutokana na tukio hilo mashabiki wake wamejitokeza kummwagia sifa wakisema jambo hilo haliwezi kufanywa na wasanii wakubwa, lakini yeye ameweza.

## Surviving R Kelly yang'ara MTV

IMEWASHANGAZA wengi! Hivi ndivyo inavyozungumzwa mitaani baada ya kufahamika filamu ya "Surviving R Kelly" iliyoachiwa rasmi Januari 3, 2019 ya mkongwe wa muziki wa RnB Robert Kelly imeshinda tuzo ya "Best Documentary" kwenye tuzo za filamu za MTV za mwaka huu.

Filamu hiyo ambayo iliibua maovu mengi ya mwimbaji huyo na kuchafua kazi yake ya muziki na kuibuka kwa tuhuma za unyanyasaji wa kingono kwa wanawake 10 waliokuwa chini ya umri wa miaka 18, ambapo R. Kelly mwenyewe amekana kuhusika.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka TMZ, filamu hiyo imeangaliwa na watazamaji zaidi ya milioni 22 katika mtandao wa You Tube.





## Chris kuitwa baba kunanoga

STAA wa muziki wa RnB, Chris Brown anatarajia kupata mtoto wa pili na aliyekuwa mpenzi wake mwanamitindo Ammika Harris ambaye ameripotiwa kuwa na uhusiano miezi kadhaa.

Baada ya kuibuka kwa taarifa hiyo, mpenzi wa sasa wa Chris Brown ambaye ni Indyamarie Jean Pelton ameamua kuachana na staa huyo.

Mwanamuziki huyo ana mtoto mwingine wa kike aanayeitwa Royalty ambaye alizaliwa mwaka 2014 na mwanadada Nia Guzman mwenye uraia wa Brazil.

## Gray wa Empere matatani

JINAMIZI baya bado linawaandama wasanii wa filamu ya Empere, safari hii ni zamu ya Bryshere Gray, ambaye amekamatwa na polisi kwa kuendesha gari bila kibali.

Kulingana na mtandao wa TMZ, nyota huyo alikamatwa Juni 13 wakati akipita barabara ya Michigan Avenue Magazine, Chicago kinyume na taratibu ya udereva.

Katika taarifa za kipolisi zinaeleza Gray alikuwa akiendesha gari aina ya Rolls Royce bila kuwa na leseni ya udereva.



SAFU



Na John Juma
0716217615

Mionzi ya Sheria

# Fahamu ilivyo likizo ya mfanyakazi, malipo yake

AWALI ya yote, ni vema ikaeleweka mapema kuwa likizo zote anayepaswa kupatiwa/kufaidika ni kila mwajiriwa aliyefanya kazi zaidi ya miezi sita mfululizo, au kama alifanya akatoka halafu akafanya tena basi hizo siku zikizidi miezi sita, atakuwa na haki ya kupata likizo.

Tunapoongelea likizo, tuna maana ile yenye malipo. Siyo mwajiri anampatia mfanyakazi likizo lakini mshahara haumpatii. Hiyo ni kinyume cha Sheria elekezi.

Binadamu kwa kawaida katika maisha na shughuli zetu, tunakutana na mengi sana ikiwa ni pamoja na magonjwa, misiba, msongo wa mawazo na vitu vingine vingi.

Mathalani, katika hali ya kawaida binadamu hatuwezi kufanya kazi miezi yote 12 bila ya kupumzika.

Mfanyakazi anahitaji likizo ili aweze kupumzisha mwili na akili yake; kuachana kwa muda fulani na mizunguko au kazi za ofisini za kila siku.

Kimsingi, makala hii iko kumsaidia mwajiri na mwajiriwa kujua jinsi ya kutoa na kuomba likizo kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Namba 6 ya Mwaka 2004, Kila mmoja kwa nafasi yake.

Sheria husika inatoa mwongozo wa jinsi ya kutoa likizo na aina ya likizo ambazo mwajiriwa anapaswa kupatiwa/ kufurahia.

Kwa kutilia mkazo zaidi hapa, kama ambavyo nimetangulia kugusia awali, likizo zote anayepaswa kupatiwa/kufaidi ni mfanyakazi/mwajiriwa aliyefanya kazi kwa zaidi ya miezi sita mfululizo; au kama alifanya akatoka halafu akafanya tena basi hizo siku, zikihesabiwa, zisizidi miezi sita atakuwa na haki ya kupata likizo kama sheria inavyotaka.

Isitoshe, tunapoongelea suala zima la likizo; hii ina maana, likizo yenye malipo. Na siyo kinyume na utaratibu huu.

**AINA ZA LIKIZO;**
**LIKIZO YA MWAKA (Annual Leave),**

Hii ni likizo ya siku 28; ambazo mfanyakazi/mwajiriwa anapaswa kuipata/kuifaidi kila mwaka.

Haijalishi mhusika yuko sekta gani; binafsi au serikalini. Hali kadhalika, wadhifa wake; mlinzi, dereva au mfanyakazi wa ndani.

Endapo wahusika watakubaliana kuwa badala ya kwenda likizo mfanyakazi/mwajiriwa aendelee kufanya kazi, basi mshahara wake wa mwezi mmoja atatakiwa kulipwa mfanyakazi/mwajiriwa huyo: Kifungu cha 31(1)-(10) cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

**LIKIZO YA UGONJWA (Sick Leave),**

Hutolewa kwa mgonjwa ambaye ni mfanyakazi/mwajiriwa kwa siku 126; siku 63 ni mshahara wote na siku 63 zinazofuata nusu mshahara.

Hata hivyo, mhusika hatoweza kupatiwa/kufaidi likizo hii endapo atashindwa kutoa uthibitisho rasmi kutoka kwa daktari au endapo inahusisha mafao kutoka kwenye makubaliano ya pamoja au hata kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Uthibitisho wa daktari ni uthibitisho wa kutoka kwa daktari aliyesajiliwa na serikali: Kifungu cha 32(1)-(4) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya mwaka 2004.

**LIKIZO YA KIFO (Compassionate Leave),**

Ni maalum kwa mfiwa. Endapo mfanyakazi atafiwa na mtu wake wa karibu; baba, mama, dada, mke, mtoto.

Atakuwa na haki ya kupata likizo ya siku nne, hutolewa pia, endapo mfanyakazi/mwajiriwa anauguliwa na mtoto mdogo.

Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 34(1)-(3) cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004.

**LIKIZO YA UZAZI (Maternity Leave),**

Likizo ya uzazi kwa mwanamke (Maternity Leave), ni maalumu kwa kinamama. Mama anapaswa kupata likizo ya siku 84 na endapo ikiwa mhusika atajifungua watoto mapacha, basi anapata likizo ya siku miamoja (100).

Sambamba na kupatiwa muda wa saa mbili (2) ya muda wa kazi kila siku kwa ajili ya kumnyonyesha mtoto/watoto wake.

**MUHIMU**

Mathalani, mtoto akifariki ndani ya mwaka mmoja (1) mhusika atatakiwa kupatiwa likizo ya uzazi tena; endapo atashika mimba nyingine.

Na zaidi sana, taarifa ya likizo husika itatolewa kwa mwajiri ndani ya miezi mitatu (3) kabla, juu ya lini likizo husika inachukuliwa.

Mama anayenyonyesha haruhusiwi kufanya kazi zinazohatarisha afya yake na ya mtoto/watoto wake.

Mama mjamzito anaweza kuchukua likizo yake wakati wowote, wiki nne (4) kabla ya kujifungua; lakini inaweza kuwa mapema zaidi endapo daktari atathibitisha hilo: Kifungu cha 33(1)-(11) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na. 6 ya mwaka 2004.

**LIKIZO YA UZAZI (Paternity Leave)**

Hii ni likizo maalumu kwa wanaume ambao wake zao wamejifungua. Ni likizo ya siku tatu na inapaswa kuchukulia ndani ya siku saba kutoka mke ajifungue.

Hatua ya msingi ni mwajiri kutaarifiwa mapema na uthibitisho kuwa aliyejifungua ni mke halali: Kifungu cha 34 (1)-(3) cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini na.6 ya Mwaka 2004.

Mwisho, haki ya likizo ni ya wafanyakazi/waajiriwa wote (kama sheria inavyoelekeza na kutaka); pia ni marufuku mwajiri kumfukuza/kumfuta kazi mfanyakazi/mwajiriwa wakati wa/yupo likizo. Naomba kuwasilisha.



Reubeni Lumbagala

Kalamu ya Mwalimu

# Wananchi nguzo muhimu ujenzi wa miundombinu ya elimu - 2

TUNAENDELEA na mwendelezo wa makala niliyoanza kuichambua juma lililopita. Juma lililopita nilieleza kwa kina kuhusu umuhimu wa miundombinu bora ili kuchochea ukuaji wa taaluma na ufaulu wa wanafunzi shuleni. Kutokana na umuhimu wa mazingira bora na yenye kuvutia katika ufundishaji na ujifunzaji wenye tija, uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya elimu kama madarasa, ofisi, nyumba za walimu, mabwalo, mabweni, vyoo bora ni jambo la kupewa uzito mkubwa.

Nilieleza pia namna wananchi wanavyopaswa kuunga mkono juhudi kubwa za serikali katika kuhakikisha mazingira na miundombinu inakuwa bora na yenye kuchochea ukuaji wa taaluma. Wananchi wanaweza kuunga mkono juhudi za uboreshaji wa miundombinu ya kutolea elimu kwa kutoa nguvu kazi, michango ya vitu na hata fedha zao. Suala la uboreshaji na ujenzi wa miundombinu bora ya shule ni jukumu letu sote na si kuiachia serikali pekee. Nilianza kuelezea namna wananchi wa Wilaya ya Kongwa walivyojitolea nguvukazi, hali iliyosababisha serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi ili kufanikisha kukamilishaji wa maboma ya madarasa. Mifano zaidi ya wananchi wa Kongwa walivyojitolea kuunga mkono ujenzi wa miundombinu bora ya elimu ni kama ifuatavyo:

Katika Kata ya Chitego wilayani Kongwa, wananchi kupitia Mfuko wa Elimu Chitego wamechangia milioni 41 ambazo pamoja na kazi za mikono yao wanajenga vyumba sita vya madarasa vya Shule ya Msingi Chitego, vyumba vitatu katika Shule ya Msingi Wangazi na nyumba ya mwalimu. Pia wameanzisha msingi kwa ajili ya vyumba vitatu. Wananchi hao pia wanajenga sekondari yao mpya na tayari vyumba vinne viko kwenye hatua ya renta na wana matofali zaidi ya 1600. Kutokana na kazi kubwa inayofanywa na wananchi wa Kata ya Chitego, Halmshauri ya Wilaya ya Kongwa imeamua kuwaunga mkono kwa kutoa milioni 42, huku Mbunge wa Kongwa ambaye pia ni Spika wa Bunge Job Ndugai akiahidi kupeleka mabati, nondo na fedha kukamilisha miradi hiyo. Katika Shule ya Msingi Mwidonya wilayani Kongwa, wananchi walitoa nguvukazi zao katika kuchimba msingi, kusomba mchanga, kokoto, ili kufanikisha ujenzi wa madarasa mawili. Kutokana na kazi kubwa, serikali ikawaunga mkono kwa kuwapa Sh. milioni 30 iliyosaidia kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo viwili. Kama hiyo haitoshi, wananchi hao hao waliendelea kutoa nguvukazi zao kuanzisha ujenzi wa darasa jingine, darasa hilo limefikia hatua za kupauliwa, huku kenchi zikiwa zimeshapigiliwa. Kazi iliyobaki ni kupiga bati tu.

Vilevile, wananchi wa Kata ya Makawa walishiriki kikamilifu katika ujenzi wa maboma ili madarasa mawili ya Shule ya Msingi Majengo yaweze kupatikana. Kutokana na juhudi zao hizo, serikali iliwaunga mkono kwa kuwapa shilingi milioni kumi na mbili na laki tano kukamilisha madarasa hayo.

Sambamba na hilo, Shule ya Msingi Visumi ilipata maboma matatu kutokana na juhudi kubwa za wananchi. Ambapo kwa kazi hiyo nzuri, Chama cha Walimu (CWT) wilayani Kongwa ilichangia milioni mbili na laki mbili na Mbunge Ndugai alitoa bati 52 kusaidia umaliziaji wa maboma hayo.

Wananchi wa Kata ya Mtanana wametoa nguvukazi zao ili kusaidia ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Shule ya Msingi Ndalibo kwa kujenga madarasa mawili. Wamejitolea kuchimba msingi, kufyatua matofali na kuinua boma. Kutokana na kazi hii, Mbunge Ndugai alitoa milioni 4 zilizosaidia kukamilisha ujenzi huo. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ndalibo, Nyanje Nyanje ametoa shukrani zake za pekee kwa Mbunge Ndugai kwa msaada alioutoa katika ukamilishaji wa madarasa. Mwalimu Nyanje alisema; "Namshukuru sana Ndugai kwa kuwaunga mkono wananchi wake ambao wamejipambanua kuwa na uelewa mkubwa wa dhana mzima ya ushiriki wa shughuli za maendeleo kwani ushiriki wao umeleta manufaa kwa ustawi wa ukuaji wa taaluma. Pia wananchi wameweza kutoa tafsiri sahihi ya shule kuwa shule ni jamii na jamii ni wao."

Kitongoji cha Chimehe, wananchi walisomba mchanga, kokoto, maji, kuchimba na kujenga msingi wao wenyewe. Kutokana na hali hii, Mbunge wa Kongwa Job Ndugai alichangia saruji mifuko 30, ambapo mabalozi wa vitongoji kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo yao walifyatua matofali wenyewe na kujenga hadi kufikia ngazi ya renta, ambapo serikali ilimalizia sehemu iliyobakia na hivyo kufanya mradi huo wa madarasa mawili kukamilika.

Ni wajibu wa wananchi kutambua mchango wao katika maendeleo ya sekta mbalimbali na elimu. Ni wakati wa wanafunzi kujifunza katika mazingira bora, kazi ibaki kwao tu-kusoma kwa bidii. Tafakari.

Jumamosi ijayo nitaendelea kuelezea namna wananchi wa mikoa mbalimbali nchini walivyoitikia wito wa kutoa nguvukazi katika ujenzi wa miundombinu ya elimu na namna serikali ilivyowaunga mkono katika ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi shuleni. Usikose.

**Maoni: (+255) 764 666349.**

KUELEKEA UCHAGUZI

# Siri rushwa ya ngono ‘

- Waliopoteza ndoa wafunguka kilicho
- Mchuano mtu na wifi, mume achukua
- Walioishiwa fedha na simu za ‘tukuta
- Takukuru Shy yatangaza kujipanga ‘k

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DEMOKRASIA ni mfumo wa kiutawala ambao wananchi wanakuwa sawa katika kusaka haki, vivyo hivyo katika misingi yote ya utawala bora.

Hata hivyo, kumekuwapo sera na misimamo potofu ya kijinsia inayokiuka usawa, hata katika baadhi ya maeneo na matukio, yanayotweliwa na mazingira ya wanaume kupendelewa zaidi kwa matendo na fursa.

Kwa kurejea demokrasia na uongozi, kumekuwapo na shuhuda mbalimbali, hata baadhi kufikia hatua ya kuwaita kinamama ‘ni viumbe dhaifu.’

Kutokuwapo usawa wa kijinsia katika nafasi za kugombea uongozi kwenye uchaguzi mbalimbali nchini, kuanzia ngazi za chini serikalini, kumechangia kupunguza idadi ya kinamama kwenye vyombo vya maamuzi.

Ni mtazamo unaokwaza nguvu za kupitisha hoja zao za kupitisha hoja. Cha kujiuliza, kwanini wanakwama?

Rushwa ya ngono

Tatizo la rushwa ya ngono kwa wagombea wanawake nchini, limekuwa kilichukua sura mithili ya ‘kitu cha kawaida.’ Ni kitu ambacho kimekuwa kikikandamiza nafsi za kinamama, katika kutimiza azima hiyo.

Ni jambo linaloonekana kawaida, wengi wamekuwa wakitoa rushwa hiyo, ili kupata fedha za kuendeshea kampeni nafasi za uongozi.

Aidha, rushwa hiyo imesababisha baadhi ya wagombea wanawake kuibua migogoro inayuhusu uhusiano ndani ya ndoa zao, vivyo hivyo kwa waume katika nafasi zao.

Mwaka huu, kufanyika uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, unaotarajiwa kufanyika Oktoba. Hapo inagusa vyeo kama vile wenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijiji, huku mwakani ikiwa ni kinyang’anyiro cha kusaka Rais, wabunge na madiwani.



Mwanaharakati wa TGNP Mtandao, Natunjwa Mvungi, akiwahamasisha wanawake wa Shinyanga kujitokeza kugombea nafasi za uongozi, kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

Katika maeneo mengi nchini, bado rekodi ya wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi haiko juu. Moja ya sababu inaangukia katika mtazamo wa kuwapo mfumo dume.

Ni mantiki inayotawalia na hali ya kinamama, kutojiamini, kukumbwa na vitisho, ukosefu wa fedha za kuendesha kampeni, kuombwa rushwa ya ngono, pia mila na desturi za wanaume, hawakubali kuongozwa na wanawake.

Kinamama waliogombea

Sarah Njabuyaga mkazi wa Chibe katika Manispaa ya Shinyanga. Huyo ni miongoni mwa wanatoa ushuhuda wa kuwahi kuombwa rushwa ya ngono na hata ndoa yake, kutokana na kugombea nafasi ya uongozi, kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014.

Mwanamama huyo anasema, nafasi ya mwenyekiti wa mtaa, huku katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aligombea udiwani wa viti maalumu.

Anasema, pindi alipotangaza nia ya kugombea udiwani wa viti maalumu, alijikuta akichukua fomu yeye pamoja wifi yake.

Ni hali anayoeleza kwamba, ilimkoseka msaada wa kifedha za kuendesha kampeni kutoka kwa mumewe, kwa sababu aliamua kumpendelea dada yake.

“Mtu yeyote anapoingia kwenye kinyang’anyiro cha kugombea uongozi, lazima uwe na rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha kampeni,” anasimulia Sarah na kuongeza:

“Kutokana na mimi kutokuwa vizuri kiuchumi na mume wangu kanitenga, kuna baadhi ya wanaume walijitokeza kuniomba rushwa ya ngono ili wanipatie fedha nami nikagoma.

“Lakini kutokana na kukubalika na kinamama sikukata tamaa, sababu baba yangu alikuwa akiniunga mkono nikaendelea kupambana na wifi yangu.

“Hadi kufikia hatua ya kuvunjika kwa ‘mji’ wangu hadi leo sina mume, sababu ya kutaka tu uongozi, ili niweze kupata nafasi ya kuyasemea matatizo ya wanawake wenzangu na kukatuliwa.”

Sarah anasema, kugoma kwake kutoa rushwa hiyo ya ngono na ukosefu wa rasilimali fedha, kulimfanya akose nafasi hiyo ya udiwani viti maalumu, aliambulia nafasi ya ujumbe wa serikali ya mtaa, ambao, hata hivyo hakuiomba.

Anasema pamoja na historia ya changamoto hizo zote, bado hajakata tamaa, kujitosa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu. Ameshatangaza nia tena ya kugombea Uenyekiti wa Mtaa wa Chibe, katika Manispaa ya Shinyanga.

Pia, shuhuda mwingine ni Rachel Madundo, mkazi wa Songwa wilayani Kishapu, Shinyanga. Huyo ni miongoni mwa wagombea wanawake wenye ufafanuzi kulikoni wanaombwa rushwa ya ngono, kupitia kampeni za uchaguzi.

Anasema, ukosefu za fedha za kuendeshea kampeni, unachangia wanawake kuombwa rushwa ya ngono, huku baadhi yao anawataja kuwa na tabia ya kupenda vitu kirahisi na kuamua kutoa rushwa, ili wapatiwe nafasi ya uongozi.

“Wakati nikigombea nafasi fulani za uongozi kwenye chama changu sipendi kukitaja, nilikuwa sina fedha za kuendesha kampeni.

“Lakini, ghafla nikapigiwa simu na mmoja wa viongozi akiniomba tukutane ‘gesti’ ili nimpatie rushwa ya ngono, aweze kunipatia fedha na kunipigia debe nipate nafasi hiyo,” anasema Madundo.

“Tatizo la rushwa ya ngono kwenye uchaguzi ni kubwa sana. Nimeshuhudia wanawake wengi tu ambao wanajitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wakiombwa rushwa ya ngono, licha hata wengine kuwa na uwezo wa kifedha. Lakini, ili upate uongozi, lazima ufanye mapenzi na mmoja wa kiongozi, tofauti na hivyo huwezi kushinda,” ameongeza.

Mwingine mwenye ushuhuda wa simulizi wa namna hiyo ni Kagwa Limbu, kupitia CCM katika uchaguzi wa kiti cha udiwani mwaka jana, katika Kata ya Kiloleli wilayani Kishapu, Mkoa wa Shinyanga.

Analieleza hilo kuwa moja ya changamoto inayowafanya kinamama wasite kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kwa kiasi kikubwa wakiri kukabiliwa na madai ya rushwa ya ngono, hali



Rachel Madundo, mkazi wa Kishapu, akiwasimulia wenzake kuhusu rushwa ya ngono alipogombea uongozi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita.



Sarah Njabuyaga, mkazi wa Chibe, Manispaa ya Shinyanga, alivyokutana na changamoto, alipogombea uongozi kwenye uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa.

## SERIKALI MTAA...

# 'yadadavuliwa' ilivyo

## wakuta
## a upande
## ane gesti'
## kininja'



Wanawake wa mkoa wa Shinyanga, wanaowania kugombea uongozi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, wakiwa katika semina iliyoandaliwa kwa ajili yao, mjini Shinyanga.

inayowarudisha nyuma katika ndoa zao.

Kagwa anasema, imekuwa kawaida inapotokea mwanamke anakubalika zaidi kwa wananchi, pia kuwa na uwezo mzuri kifedha katika kuendesha kampeni, bado ushindi katika kampeni kwake inakuwa vigumu.

"Lazima tu uombwe rushwa ya ngono na usipokuwa na msimamo, lazima ataitoa tu ili mradi upate uongozi," anasema.

"Wakati nikitafuta kura za maoni za kuteuliwa na chama changu cha CCM kuwa mgombea wa udiwani katika kata ya Kiloleli, nilikuwa nikipambana na wanaume wanawake, nikawashinda

"Cha ajabu, wakahamia upinzani ili kushindana na mimi na wakanishinda kutokana na kutumia pesa nyingi," anasema Kagwa.

Anasimulia mkasa wa kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi, akisema: "Wakati nikiwa kwenye harakati hizo za kutafuta nafasi hiyo ya udiwani nilikumbana na changamoto nyingi sana, ikiwamo kuombwa rushwa ya ngono.

"Kutokana na misimamo yangu, hawakuweza kufanikiwa. Pia, nilikuwa nikipata msaada wa kifedha kutoka kwa mume wangu," anasema.

Maryana Buhama, ni mwanaharakati wa kupigania haki za wanawake mkoani Shinyanga, kutoka kikundi cha Ujirani Mwema.

Wanaharakati

Anasema kupitia miezi iliyosalia kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, kunapaswa kutolewe elimu sahihi ya kutokomeza rushwa hiyo ya ngono kwa wanawake waogombea wa nafasi mbaimbali za uongozi.

"Tatizo ambalo linasababisha rushwa hii ya ngono kuendelea kuwepo kwenye chaguzi mbalimbali ni ukosefu tu wa elimu, ambayo ikitolewa ipasavyo na kuhakikisha wanawake wengi tu watajitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi licha ya kutokuwa na rasimali fedha za kutosha kwa ajili ya kampeni," anasema Buhama.

Othumani Ndamo, mkazi wa Kishapu anasema katika nafsi yake, anapenda sana wake zake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, lakini linapokuja suala la rushwa ya ngono, huwa linampa ukakasi.

Ushauri wake kwa kinamama ni kwamba, wanapotaka kutangaza nia, wanapaswa kuwashirikisha waume zao kwanza. Anaendeleza simulizi:

"Mimi mke wangu akitaka kugombea nafasi yoyote ya uongozi, lazima anishirikishe kwanza, ili nione namna ya kumsaidia kifedha kuendesha kampeni na kumwepusha kuombwa rushwa ya ngono."

Mwingine mwenye maoni katika mukatadha huo ni mwanaharakati kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Natunjwa Mvungi, anasema wamekuwa wakiendesha mafunzo ya kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi, ili kufikia malengo ya '50 kwa 50.'

Natujwa anasema kuwa, bado kuna idadi ndogo ya wanawake viongozi hasa kwenye vyombo vya maamuzi nchini, akieleza hoja yake kwa kauli:

"Mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, kwa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014 na uchaguzi mkuu 2015, wenyeviti wa vitongoji walichaguliwa wanaume 660, wanawake hakuna, vijiji wanaume 116 wanawake mmoja, madiwani wanaume 23, wanawake wawili.

"Hii ni picha ambayo inaonyesha kuwa wanawake bado ni wachache kwenye nafasi za uongozi hapa nchini. Wanahitaji kuhamasishwa kugombea uongozi, ili kuwapo usawa na hasa kwenye vyombo vya maamuzi, katika kuwasilisha matatizo yao na kutatuliwa," anaeleza Mvungi.

Pia, ana ushauri kwa kinamama wajiunge kwenye vikundi vya ujasiriamali, ili wapate mikopo kwenye halmashauri zao wanakotengewa bajeti asilimia nne za mapato ya ndani.

Natujwa anasema, fedha ambazo zitawasaidia kuwapatia mitaji na kufanya biashara, jambo ambalo mustakabali wake ni kuwaepusha kinamama na vishawishi vya rushwa ya ngono.

### Bosi Takukuru

Kaimu Mkuu wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Shinyanga, Francis Luena, anawataka wanawake wagombea, pindi wanapoombwa rushwa ya ngono, wafike kwenye taasisi hiyo kutoa taarifa, ili wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Luena anasema, Takukuru imeshafungua dawati la kushughulikia masuala ya rushwa ya ngono na kuna maofisa maalumu wa kike watakaokuwa wakipokea taarifa hizo na kuzifanyia kazi.

Raia yake ni kwamba, wagombea kinamama watumie nafasi hiyo, ili kumaliza changamoto iliyopo.


"Natoa wito kwa wagombea wote wanawake mkoani hapa wale ambao wataombwa rushwa ya ngono kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, wasisite kuja kutoa taarifa kwetu, ili tupate kulimaliza tatizo hili ambalo linawadhalilisha na kuwanyima haki zao," anasema Luena.

Pia, anaeleza mikakati iliyopo kwenye taasisi hiyo ni kuendelea kutoa elimu hiyo ya rushwa ya ngono kwa kutembelea shuleni, vyuoni, sokoni, minadani na kwenye mikusanyiko ya watu, ili wapate taarifa za rushwa hiyo, ikiwea ni nammna bora ya kukomesha jambo hilo ndani ya Shinyanga.



Wanawake kutoka maeneo tofauti ya Mkoa wa Shinyanga, wakijadili kwenye vikundi, changamoto zao wanapotangaza nia ya kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi, ikiwamo rushwa ya ngono. Kikao hicho kilifanyika katika Manispaa ya Shinyanga.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 6 00)



**Dondoo: Kulia**

1.Mlimaji mkuu wa mahindi
7. Mti mgumu
8. Jiji la Miamba 9. kitu chenye uhai na majani
11.Kataa kutii sheria za nchi
12.Utaratibu wa kununua au kuuza bidhaa 14. dutu
15.Piga ramli
18.Kiongozi wa Ujerumani
20.Mionzi ya mwanga
22.Ondolewa maganda
24.podo 27.Chagua watu/vitu 28.kinywaji 29.Mji mkuu Muscat 31.mapatano
32.Balaa 33.Kitowe

**Dondoo: Chini**

1. Bandari kubwa Kenya
2. Pesa ya Omani
3. Ukoo
4. Kiongozi wa sala msikitini
5. Mlima ambako Musa alipokea amri kumi
6. Mtu asiyezaa
9. Ndege mkubwa asiyeruka
10.songa mbele 13.lalia mayai
14. kitu cha kuliwa 16. bei
18. Banjul ni mji wake mkuu
19.dhamira 21.tendo la kujikwaa
23.Pepesuka 25.Watu wa Peru
26.Mtaa
30.zao la nyuki

## Jibu Na: 5

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Z | U | M | B | U | K | U | K | U | ■ | U | ■ | M |
| A | ■ | A | ■ | T | ■ | Z | ■ | G | ■ | Z | ■ | L |
| M | A | M | L | A | K | A | ■ | A | K | I | L | I |
| B | ■ | A | ■ | N | ■ | O | S | L | O | ■ | ■ | M |
| E | ■ | ■ | ■ | G | ■ | ■ | H | I | M | A | Y | A |
| Z | I | M | B | A | B | W | E | ■ | E | ■ | ■ | N |
| I | ■ | W | ■ | Z | ■ | ■ | R | I | S | A | S | I |
| ■ | K | I | P | A | N | D | E | ■ | H | ■ | A | ■ |
| U | ■ | M | ■ | J | ■ | ■ | H | I | A | R | I | ■ |
| N | A | B | I | I | ■ | ■ | E | ■ | ■ | ■ | D | ■ |
| E | ■ | A | ■ | ■ | M | ■ | ■ | N | U | B | I | A |
| N | ■ | J | A | M | B | A | Z | I | ■ | ■ | W | ■ |
| E | ■ | I | ■ | ■ | U | ■ | ■ | A | N | D | A | A |

MAKALA

# TALA; Jukwaa linalochagiza mafanikio urasimishaji ardhi

**Na Mashaka Mgeta,**
MOROGORO

PROGRAMU ya kupima ardhi (LTSP) inayofanyika katika wilaya za Ulanga, Malinyi na Kilombero mkoani Morogoro, inaibua mafanikio yanayochagizwa na ushiriki wa Jukwaa la Wadau wa Ardhi nchini (TALA).

Wakati serikali ikishiriki kutekeleza upimaji na urasimishaji ardhi, TALA kupitia wadau wake wanaofanya kazi katika maeneo ya sheria, haki za mwanamke na makundi maalum kama wafugaji, wamejikita zaidi katika uelimishaji jamii, uhamasishaji na ufuatiliaji.

Hata hivyo, licha ya ushiriki mpana, weledi na ujuzi kwa maeneo ya uelimishaji na uhamasishaji jamii, asasi hizo zilianza kutekeleza shughuli zao baada ya sehemu kubwa ya upimaji na umilikishaji ardhi kufanyika.

Meneja wa Programu wa TALA, Jamal Omar, anasema kuchelewa kwa asasi hizo kushiriki katika mradi huo hakujasababisha athari zinazozidi manufaa yake.

**HUDUMA HAIJAWAFIKIA MAELFU**

Kujumuishwa kwa asasi hizo kunatajwa na wadau wa programu hiyo kuwa ni chachu ya kuongeza uelewa wa wananchi, kwa vile uelimishaji na hamasa inayofanywa na halmashauri za wilaya wakati wa upimaji, vilikabiliwa na ufinyu wa muda na upungufu wa rasilimali, hivyo kutoeleweka vema kwa wananchi.

Pia, pamoja na manufaa yanayoonekana kupitia ushiriki wa TALA, idadi ya watu wanaofikiwa inatajwa kuwa ni ndogo ikilinganishwa na ukubwa wa mahitaji ya wakazi kwenye maeneo ya mradi wa LTSP.

Kwa mfano, Ofisa Upimaji katika wilaya ya Ulanga ambaye hataki jina lake kutajwa gazetini, anasema kati ya vijiji 52 vilivyopo wilayani humo, 12 bado havijapimwa, vinne vina migogoro inayotokana na kuchangia mipaka na vinane vipo katika mchakato wa ardhi yao kupimwa.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Ulanga, Libert Kanyakanya, anasema kwa mazingira ya kijamii yaliyopo wilayani humo, ni dhahiri kwamba uelimishaji, ushawishi na utetezi unaofanywa na asasi hizo kupitia TALA, vilipaswa kufanyika kabla ya upimaji na urasimishaji ardhi.

Kanyakanya aliyeshiriki uhamasishaji jamii kupima ardhi anasema uhamasishaji huo ulifanyika kwa kiwango kidogo kupitia timu ya ushirikishaji matumizi ya ardhi.

Kwa mujibu wa Kanyakanya, bado kuna pengo kati ya huduma za uelimishaji na uhamasishaji kwa upande mmoja na idadi ya watu waliofikiwa kwa upande mwingine.

"Kwa wenzetu hawa (TALA) wanatumia muda mrefu zaidi kukaa na wananchi, wana wataalamu wa kutosha katika masuala yanayohusiana na ardhi hivyo ni muhimu wakaongeza maeneo na idadi ya watu wa kuwafikia," anasema.



Mratibu wa Programu wa TALA, Jamal Omar (wa pili kulia), akizungumza na Ofisa Miradi wa Caritas katika Jimbo Katoliki la Mahenge, Anastazia Shimbili (kushoto). Wengine pichani ni watumishi wa Caritas, Mratibu wa Kilimo Endelevu, Thadei Dulle na ofisa anayeshughulikia masuala ya fedha, Julitha Mhumpa. **PICHA: MASHAKA MGETA**

**CHANGAMOTO**

Kanyakanya, anasema licha ya asasi hizo kuhitajika, lakini zipo changamoto katika utendaji kazi wao hasa kwa kushindwa kuvifikia vijiji vilivyopo mbali kutoka makao makuu ya wilaya.

"Inawezekana ni kutokana na upungufu wa rasilimali, lakini ni vema changamoto hii wakaielezea kwenye miradi yao ili waifikie jamii nyingine zaidi ya hizi za vijiji vya karibu na halmashauri," anasema.

Kanyakanya anasema kadri anavyotembelea maeneo ya vijiji vilivyonufaika kwa uelimishaji unaofanywa na washirika wa TALA, amebaini kuwapo mwamko na uelewa mkubwa wa masuala yanayohusiana na upimaji na umilikishwaji ardhi.

"Kabla ya mradi huu watu wa vijijini hawakujua thamani ya ardhi, lakini baada ya kufikiwa na uelimishwaji kutoka TALA, kiwango cha hamasa na uelewa kimeongezeka," anasema.

Pia Kanyakanya anasema ushirikishwaji wananchi kwenye mafunzo ya TALA, kumeimarisha mwamko wao kujitokeza katika masuala mengine yanayohusu maendeleo ya jamii.

Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mahenge, Venance Huruma, anaunga mkono kutanua wigo wa elimu na uhamasishaji jamii unaofanywa na TALA, akitoa mfano wa mmoja wa washirika wake, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kilivyofanikisha kutoa elimu wilayani humo.

Huruma, anasema TAWLA inayoelimisha zaidi kuhusu haki za kisheria kwa mwanamke katika kumiliki ardhi, imefanya kazi kwa awamu mbili, moja ikivifikia vijiji 10 na nyingine vijiji 20.

Pia, Huruma analitaja shirika lisilo la kiserikali la PINGOs lililo pia mshirika wa TALA, kwamba limefanikiwa kuielimisha jamii ya wafugaji umuhimu wa matumizi bora ya ardhi.

"Inawezekana kuna wengine pia walishafikia, lakini wito wangu ni kwamba wanaokuja wasiende huko vijijini moja kwa moja, wafike kwenye serikali ya wilaya ili watushirikishe tunaoratibu manufaa yanayotokana na shughuli zao," anasema.

Naye Ofisa wa Mipango ya Ardhi wilayani humo, Ole Mungaya, anasema muda mfupi na rasilimali chache vilichangia kufifisha mafunzo ya uelimishaji na uhamasishaji jamii kabla ya upimaji wa ardhi.

"Kwa hiyo msisitizo wa awali ukawa ni kuwaelimisha wanavijiji, angalau waelewe umuhimu wa kupata hati miliki za maeneo yao," anasema.

Mahitaji ya kutanua wigo huo yanatajwa pia na Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Nakafulu wilayani Ulanga, Mwalimu Paschal Laurent, anasema elimu hiyo itatumika kama nyenzo ya kudai na kupigania haki za ardhi.

Steven Zayumba ni Ofisa Mpimaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, anasema mpango wa kuelimisha kuhusu LTSP unapaswa kutekelezwa kwa muda mrefu zaidi, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali na wataalamu waliopo.

Anatoa mfano jumla ya vijiji 23 kati ya 33 vilivyopo kwenye wilaya hiyo, ukiondoa saba vilivyoingizwa kwenye eneo la mjini, ndivyo pekee vimefikiwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, wakati 16 pekee vimepimwa na wakazi wake kurasimishwa ardhi.

**MAFUNZO YA TALA**

Asasi zinazounda TALA zinashiriki kutoa mafunzo katika maeneo tofauti kwa kuwafikia walengwa wa mradi wa LTSP katika wilaya hizo.

Mathalani, Jumuiko la Rasilimali Tanzania (TNRF) na Taasisi ya Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT), vimefikia wakazi wa vijiji vitano katika Wilaya ya Ulanga na kuwaelimisha kuhusu namna Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 ya mwaka 1999 zinavyogusa maslahi yao.

**SHERIA ZA ARDHI**

Mwanasheria kutoka TNRF, Zarubaberi Ngowi, anasema katika uelimishaji vijijini, ametumia sehemu za sheria za ardhi ili kurahisisha uelewa kwa wakazi wa maeneo hayo.

Akazitaja baadhi ya sehemu hizo kuwa ni sura ya 216 ya Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi ya mwaka 2002 iliyoagiza kuundwa kwa mabaraza ya usuluhishi wa migogoro.

Ngowi anasema kutokana na hatua hiyo, Sheria ya Ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5, zote za mwaka 1999 zikataja uwepo wa mabaraza hayo.

Mabaraza hayo ni Baraza la Usuluhishi la Kijiji, Baraza la Ardhi la Kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Ngowi, anasema uzoefu umeonyesha kuwapo uelewa mdogo wa wananchi kufuata utaratibu huo, na sababu zinazochangia ni wajumbe wake kuonekana hawana mamlaka ama baadhi ya wajumbe kukabiliwa na migogoro ya ardhi kwenye vijiji vyao, hivyo kukosa mamlaka ya kimaadili katika usuluhishi.

Baraza la Usuluhishi la Kijiji linatakiwa kuwa na wajumbe saba, angalau watatu miongoni mwao kuwa wanawake, na Baraza la Ardhi la Kata linatajwa kuwa na wajumbe wanane, wakiwamo wanawake wasiopungua watatu.

Ngowi, amezitaja changamoto nyingine zinazohitaji msaada wa kisheria vijijini kuwa ni msaada kwa wanawake wanaoishi miaka mingi kwenye ndoa kukosa haki ya kumiliki ardhi baada ya kupewa talaka.

Pia kupitia mafunzo hayo, TNRF na LEAT wanaunda timu za ufuatiliaji na uwajibikaji jamii (SAM), ili kuwapa wananchi nguvu ya kupata taarifa na mrejesho kutoka kwa watumishi wa umma na viongozi wao.

Edna Tibaijuka ni Ofisa Mazingira wa LEAT, anasema sifa za kuwa mjumbe wa SAM umri wa kuanzia miaka 18, jasiri na mwenye uwezo wa kudadisi, nguvu ya ushawishi, kujituma, kujitolea, nidhamu na mwenye akili timamu.

Kwa mujibu wa Edna, ili kufanya kazi wa ufanisi, timu hizo zinalazimika kukubalika na kuidhinishwa kisheria katika ngazi za vijiji na halmashauri husika.

"Kuna mambo tunayowafundisha, mathalani ni kuwatambua wahusika katika ufuatiliaji na uangalizi kuwa ni pamoja na Bunge, Baraza la Madiwani, Mahakama, vyombo vya habari, asasi za kiraia na jamii," anasema.

Kupitia utekelezaji huo, TNRF na LEAT zimevifikia vijiji vitano kati ya 59 vilivyopo katika Wilaya ya Ulanga, kimojawapo kikiwa ni Idunda. Kijiji hicho kimeundwa SAM lenye kamati ndogo zinazoongozwa na wenye majina yao kwenye mabano;- mipango na fedha (Zakaria Magazini), jamii (Erigi Kapelwa), ulinzi (Felix Msuhuda) na maliasili (Patrick Kaduma na Clementina Mgaya).

Wajumbe wengine ni wawakilishi wa asasi za kidini (Agripina Makuma na Cryprian Mzee) wakati wazee wanawakilishwa na John Lihamba na Magdalena Moyo.

**UMUHIMU WA UFUATILIAJI**

Kiongozi wa kamati ya mipango na fedha ya SAM kijijini Idunda, Zakaria Magazini, anasema ufuatiliaji na uwajibikaji jamii ulianza kutekelezwa kabla ya kuundwa kwa kamati hiyo ingawa kwa mfumo usio rasmi.

Anatoa mfano kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, aliyekuwa Mwenyekiti wa kijiji hicho alikaidi mara kadhaa kuitisha mkutano wa wanakijiji, ndipo wajumbe wa halmashauri yake walipokutana na kumuondoa madarakani.

Naye Edward Kapero mkazi wa kijiji hicho akasema Mwenyekiti aliyekaimishwa baada ya kuondolewa aliyechaguliwa, alibainika pia kukihujumu kijiji hicho kwa kupokea fedha kutoka kwa wafugaji, kisha kuwapa ardhi pasipo idhini ya mkutano mkuu wa kijiji.

"Tulibaini kutoa ardhi kwa wafugaji, tulipofuatilia na kuthibisha hilo, tulimuondoa madarakani, ametoweka na vifaa vya ofisi ikiwamo mihuri," anasema.

Meneja wa Programu wa TALA, Jamal anasema vifaa vya serikali katika ngazi yoyote ikiwamo kijiji, havipaswi kumilikiwa na mtu asiyekuwa kiongozi, hivyo hatua ya Kaimu Mwenyekiti huyo aliyeondolewa madarakani ni uvunjifu wa sheria.

**Mwandishi wa makala haya anapatikana kupitia 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.**

# Rais Trump asitisha kuishambulia Iran

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesitisha ghafla kuishambulia Iran muda mfupi baada ya kutoa idhini ya kufanya hivyo kujibu shambulio la Iran lililoidungua na kuiangusha ndege isiyo na rubani ya Jeshi la Marekani.

Gazeti la New York Times limeripoti likiwanukuu maofisa wa ngazi ya juu wa utawala wa Marekani, wakisema kuwa Rais Trump, aliidhinisha kufanywa mashambulizi kwa kuyalenga maeneo kama rada za jeshi na mizinga ya kufyatua makombora.

Mashambulizi hayo yalipangwa kufanyika kabla ya mapambazuko ya jana asubuhi kujibu shambulio la Iran la kuiangusha ndege ya Jeshi la Marekani kwa madai ya kuingia kwenye eneo lake la bahari.

Gazeti hilo, lilisema ofisa mmoja wa utawala wa Trump alisema ndege za kivita zilikuwa angani na meli zilijiweka tayari, lakini hakuna kombora lililofyatuliwa wakati amri ya kusitisha mashambulizi hayo ilipotolewa.

Uamuzi huo wa ghafla wa kusitisha kuishambulia Iran umezuia kile ambacho kingekuwa hatua ya tatu ya kijeshi ya utawala wa Trump katika eneo la Mashariki ya Kati baada ya kuvishambulia vituo vya Jeshi la Syria mwaka 2017 na 2018.

Hata hivyo, haijafahamika mara moja iwapo mashambulizi dhidi ya Iran yataendelea na haijawa wazi uamuzi huo wa Trump wa kuyasitisha umechochewa na kitu gani.

Hapo juzi Rais Trump, alisema Iran imetenda kosa kubwa kwa kuiangusha ndege ya Marekani katika anga ya mlango bahari wa Hormuz. Rais Trump alipoulizwa kuhusu hatua atakazochukua, alisema kwa mkato "mtafahamu hivi karibuni".

Lakini pia Trump aliashiria kuwa huenda shambulio hilo huenda lilifanywa kimakosa na mtu aliyepewa maelekezo na mamlaka za Iran.

Wakati huo huo, Iran imesema imeyapata mabaki ya ndege isiyo na rubani ya Jeshi la Marekani katika eneo lake la bahari baada ya kuidungua.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran Mohamed Javed Zarif, alisema kupitia ukurasa wa Twitter kuwa ndege hiyo ilidunguliwa baada ya kukiuka utaratibu na kuingia kwenye anga la Iran.

Katika barua kwenda Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa UN) na kwa Katibu Mkuu wa Umoja huo, Iran imelalamika dhidi ya kile ilichoita kuwa vitendo hatari na vya uchokozi vya Jeshi la Marekani kwenye eneo lake la bahari.

Marekani kwa upande wake ilisema ndege iliyoangushwa ilikuwa kwenye eneo la maji ya kimataifa.

Katika hatua nyingine viongozi wa Bunge la Marekani wametoa wito wa kuchukuliwa tahadhari kuepusha kuongezeka mvutano na baadhi ya wabunge wamesisitiza kuwa Ikulu ya Marekani inapaswa kuliarifu Bunge na kupata idhini yake kabla ya kuchukua hatua yoyote dhidi ya Iran.

*DW*



Kifungo cha nyangumi nchini Urusi. **PICHA AFP**

# Nyangumi wafunguliwa jela Urusi

**RUSSIA, Moscow**

ZAIDI ya nyangumi 100 waliopo kizuizini nchini Urusi, waanza kufunguliwa.

Kundi la nyangumi hao waliokuwa kizuizini Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo, wanaachiwa kufuatia upinzani mkali uliopazwa na sauti za wanasayansi wa bahari.

Aidha, watu mashuhuri nao wamehusika kutoka sehemu mbalimbali duniani juu ya kile kinachoitwa "jela za nyangumi".

Nyangumi hao wanashikiliwa katika vizimba vidogo vilivyotengenezwa kwenye Bahari ya Japan.

Ilielezwa kuwa wataachiliwa kwa makundi, na kazi hiyo inatarajiwa kuchukua miezi kadhaa mpaka kukamilika.

"Tumechukua uamuzi huu wa busara baada ya kushauriwa na wanasayansi kuwaachilia wanyama hawa kurudi kwenye mazingira yao ya asili ambapo walikamatwa," alisema Naibu Waziri Mkuu wa Urusi Alexei Gordeyev Alhamisi wiki hii.

"Operesheni hii itachukua kipindi cha miezi minne hivi mpaka kukamilika," alisema.

Nyangumi wanane wataachiliwa kwenye hatua ya kwanza ya operesheni hiyo. Wawili walishaachiliwa Alhamisi, alisema.

Rais Vladimir Putin, amesifia hatua hiyo katika hotuba yake ya mwaka ambapo hupokea simu kutoka kwa raia na kujibu maswali yao.

"Nyangumi hao kwa jinsi ninavyojuawana thamani ya dola milioni 100," alisema. "Linapokuwa tatizo la pesa nyingi, utatuzi wake huwa mgumu. Nashukuru Mungu mambo yameanza kusonga mbele."

Nyangumi hao wenye umri mdogo walinaswa mwaka jana kwenye Bahari ya Okhotsk.

Walisafirishwa baada ya kunaswa kwa zaidi ya kilomita 1,300 kusini mpaka katika mji wa bandari wa Nakhodka ambapo wanashikiliwa.

Japo Urusi inaruhusu kunasa nyangumi kwa shughuli za kisayansi, watafiti wana mashaka kuwa wanyama hao walikuwa wauzwe kwenye majumba ya maonyesho yaliyopo China.

Nyangumi mmoja mmoja ambao hunaswa kwa njia haramu huuzwa kwa mamilioni ya dola.

*BBC*

# EU yaipa Sudan Kusini mamilioni

**JUBA, Sudan Kusini**

UMOJA wa Ulaya, umeipa Sudan Kusini euro milioni 48.5 kuisaidia kukabiliana na changamoto za kibinadamu zinazowakumbuka mamilioni ya raia wa nchi hiyo.

Hatua hiyo inakuja baada ya Umoja wa Ulaya, wiki iliyopita, kutoa Dola milioni 1.13 kuisaidia nchi hiyo kupambana na maambukizi ya ugonjwa hatari wa ebola.

Licha ya mkataba wa amani uliotiwa saini kati ya Rais Salva Kiir na hasimu wake kiongozi wa upinzani Riek Machar mwaka 2018 baada ya mapigano tangu mwaka 2013, watu karibu 2,000,000 wameyakimbia makwao na wengine 7,000,000 wanahitaji misaada ya kibinadamu.

Mahitaji hayo hasa ni chakula na dawa.

"Umoja wa Ulaya, unaendelea kusimama na watu wa Sudan Kusini. Tunawakumbuka watu 4,000,000 ambao wanaoishi kambini, na msaada huu utawasaidia kupata misaada mingine mbalimbali," alisema Christos Stylianides, anayehusika na misaada ya kibinadamu katika umoja huo.

Fedha hizo pia zinatarajiwa kuwasaidia watu wenye uhitaji mkubwa kama watoto, wanawake na wazee ambao wanaishi kambini.

Tangu mwaka 2014, Umoja wa Ulaya umetoa Dola milioni 623, kuwasaidia wananchi wa taifa hilo ambao wamekimbia makwao kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyotikisa taifa hilo changa kwa umri barani Afrika.

**"Umoja wa Ulaya, unaendelea kusimama na watu wa Sudan Kusini. Tunawakumbuka watu 4,000,000 ambao wanaoishi kambini, na msaada huu utawasaidia kupata misaada mingine mbalimbali," alisema Christos Stylianides, anayehusika na misaada ya kibinadamu katika umoja huo.**

*Radio Ufaransa.*

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jeraha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# Jumba Jekundu-6

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

GHAFLA kuna mtu mmoja aliingia kwenye ukumbi wa kucheza muziki. Hakuna mgeni machoni mwa Kadili na mwenzake. Walimuona wapi?

Wakati anarudisha kumbukumbu nyuma na kuweza kukumbuka kuwa alikuwa ni mmoja wa mabaunsa aliowaona wiki mbili zilizopita wakimchukua msichana yule, nyuma yake aliingia mrembo ambaye amemfanya kutokuwa kwenye hali ya kawaida kwa muda wa wiki mbili sasa.

Macho ya Kadili na Meze yakagongana. Wakaangaliana. Walishindwa kuongea kitu chochote. Miguu ilianza kucheza Kadili. Mdomo pia ni kama ulikuwa umefungwa na kufuli gumu. Hakuweza kuinua hata hatua moja ya mguu.

Waliyemuona siku ile alikuwa amependeza mara kumi zaidi kuliko siku ile. Alionekama ni malkia haswa.

Kuna dhana imejengeka kuwa baada ya miaka 50, malaika mmoja hudondoka duniani. Huenda mmoja wao ni huyu. Kadili aliwaza.

Urembo, mavazi yake ya gharama yaliupamba usiku ule pamoja na ukumbi ule. Harufu mpya nzuri ya pafyumu, ilibadilisha hewa ya ukumbi ule. Kadili alijihisi kama anashindwa kuhema.

Mabausa watatu wale wale wa siku ile ya kwanza, walikaa pembeni kabisa mwa ukumbi na kumuacha binti yule akicheza disco peke yake taratibu.

Kadili alitaka kusogea katikati ya ukumbi ili acheze na kuonekana na mrembo yule, lakini miguu yake ilionekana kuendelea kutompa ushirikiano kwa kutetemeka. Alibaki amejikunyata kama mtu anayeona baridi.

Bahati ni kwamba wengi waliokuwa wakicheza hapo walikuwa na wenzi wao, ndiyo maana ilimpa fursa mrembo huyo kucheza peke yake, ingawa mibaba hiyo hiyo iliyokuwa ikicheza na wapenzi wao, ilikuwa ikiiba jicho na kumtazama mrembo huyo, wakiushangaa uzuri wake, mioyo yao ikiburudika.

Kwa mbali jicho la mrembo huyo ni kama lilimuona Kadili. Mwenyewe alibaki amesimama akiwaangalia wanaocheza, huku akijua mrembo yule ama amemsahau, au kwa siku hiyo hakuwa na mpango wowote na yeye.

Mrembo alioneka kucheza akisogea eneo lile. "Vipi swahiba, leo unaumwa." Ni sauti ambayo ilipenya si kwenye sikio la Kadili tu, lakini mpaka moyoni.

Ilikuwa ni sauti ya msichana yule ambaye alionekana kumkumbuka Kadili, lakini pia kumfuata na kwenda kumsalimia.

Kwa vyovyote ambavyo ingekuwa,




Kadili asingeweza kumfuata msichana yule na kwenda kumsalimia.

"Hapana, siumwi, ila naangalia tu watu wanaocheza."

"Siku ile ulicheza vizuri sana, leo njoo tucheze tena wote, leo na mimi nitakuonyesha kuwa najua zaidi kuliko wewe." Aliongea kwa sauti ya mzaha, iliyokuwa nyororo na tulivu.

Maneno yote yale na yaliyotokea kwa Kadili kwake ilionekana kama ni ndoto. Alibaki amesimama, kabla ya mrembo hule kumshika mkono na kumvuta katikati na kucheza naye muziki.

Meze naye alijitosa kucheza muziki, huku akimuangalia kwa chati rafiki yake aliyekuwa chini ya himaya ya mrembo ambaye hawamfahamu, lakini ni kama ameondokea kuuteka moyo wake, lakini kikwazo kikubwa kikiwa ni hadhi.

Baada ya ngoma nne, hivi, kila mmoja kicheza kwa bidii, mrembo alisogeza mdomo wake kwenye sikio la Kadili.

"Unaitwa nani?"

"Kadili."

"Ok, unaishi wapi?"

"Naishi Tandale Kwa Tumbo."

"Nashukuru kukufahamu swahiba, mimi naitwa Edina, naishi Oysterbay."

Baada ya nusu saa kupita, mabaunsa walimfuata mrembo na kumnong'oneza jambo.

"Kwa heri swahiba, tutaonana Mungu akipenda." Aliaga mrembo.

"Asante sana." Kadili aliitikia.

Hamu ilikuwa imeisha. Tayari alikuwa ameshapata alichokifuata. Amepata alichokikusudia.

Kumuona mrembo ambaye alikuwa akimkosesha usingizi. Na kwa bahati nzuri ni kwamba ni yeye mwenyewe mrembo yule ndiye aliyemwita, akampokea, akamkumbatia na kucheza naye. Ilimfariji mno Kadili. Alijiona kama anataka kuwa kama ndege apae angani. Bado hakuwa na uwezo wa kumwambia mrembo yule neno 'nakupenda' kwa sababu nyingi tu. Na pia mrembo yule hajawahi kumtamkia Kadili kuwa nakupenda.

Lakini kile tu kitendo cha kumjali, kucheza naye, kumkumbatia, kumthamini kuliko mwanaume yoyote mle kwenye ukumbi, licha ya kwamba hakuonekana kuwa na uwezo wa kipesa, kilimfariji mno kuliko faraja yenyewe.

Aliondoka na rafiki yake Meze wakiwa na furaha moyoni, wimbo mdomoni.

********************************

"Ndugu yangu sasa unakaribia kumnasa yule demu." Meze alianzisha mazungumzo muda mfupi tu baada ya Kadili kuwasili kwenye duka lake. "Mhh mimi naona kama bado na safari ni ndefu."

"Mimi ndiyo nakwambia, unajua yule demu alikuwa anacheza anatafuta yule wa siku ile yuko wapi, alipokuona nikamuona mwanangu kakufuata na kukushika mkono anakuvuta, mzee naona ukakumbatiwa."

Kikafuatiwa kicheko cha wote wawili.

"Du, ile pafyumu yake mzee baba hadi leo bado inanukie mwili mwangu." Kicheko kingine kikafuata.

"Yule demu mimi nakwambia Kadili keshamaindi nembo hiyo, ila hataki tu kukwambia, labda wewe sasa safari inayokuja umwambie." Meze alimchomekea mwenzake.

"Mhh ndugu yangu unanitafutia muhali. Labda yule demu anapenda tu kucheza na mimi kwa sababu haoni mwingine anayejua kucheza mle ndani kama mimi, lakini si kwa ajili ya mapenzi." Kadili alisema ingawa mwenyewe hakupenda iwe vile.

"Kweli mimi tangu siku ya kwanza nilipomuona nimetokea kumpenda na nashukuru ameendelea kunichangamkia na kunijali, lakini si unaona mwenyewe yule anaonekana matawi ya juu, mimi nitamuweza wapi yule?" Lilikuwa ni jibu kwa mwenzake, lakini lilionekana pia kama swali vile.

"Mapenzi yana maskini au tajiri bwana?" Meze naye alilipiza kwa staili ile ila ya swali.

"Hayana, lakini inategemea vile vile, yule si unamuona anakuja na mabaunsa. Umeshawahi kumuona demu yeyote mle kwenye disco analindwa kama yule. Nadhani kama si mtoto wa waziri au tajiri mmoja mkubwa nchini hii, kwa hiyo itakuwa vigumu sana kuwa na mtu kama mimi." Bado Kadili alijiona ni dhalili mbele ya msichana yule.

Na kweli ilikuwa hivyo kwa mwonekano wa moja kwa moja. Alionekana kuwa ni msichana anayetoka katika familia tajiri anayekuja na mabaunsa watatu wanaomuacha afurahi, lakini muda wote wanaangalia usalama wake na pia wao ndiyo wanaouangalia muda wa mrembo huo wa kukaa pale na kurejea nyumbani.

"Au atakuwa ameolewa?" Kadili aliuliza.

"Wee aolewe yule, angeolewa si angekuja na mumewe, au hata kama angekuwa na mchumba angekuja na mchumba wake pale, lakini wewe angalia, kila tukienda pale anakuja peke yake, ina maana yule anatoka nyumbani kwao kwa baba na mama yake, halafu angekuwa na jamaa yule wale mabaunsa wasingekubali wewe ukumbatiane naye." Kadili alikubaliana na maneno ya mwenzake kuwa msichana yule alikuwa akitokea kwao na kuja pale.

"Naona mzee baba demu kakuuliza hadi jina."

"Kaniuliza na yeye pia kaniambia anaitwa Edina, anaishi Masaki."

"Du Masaki na Tandale, du mwaka huu tutaona mengi." Meze alimtania mwenzake na kuangalia vicheko, kabla ya kugongeana mikono.

****************************************

Hakukuwa na mti wowote walioona maeneo hayo ambayo yangeweza kutoa kivuli cha binadamu au kiumbe hai yoyote yule kujipumzisha kutokana na jua kali.

Kutokana na hali hiyo, mama Kadili alikuwa ametandika mkeka pembeni kidogo ya nyumba yake ambako jua limeelekea na kufanya kivuli kidogo cha nyumba.

Kivuli hicho kidogo ndicho kilichomfanya mama huyo kutoa mkeka wake na kujiweka hapo akisuka ukili.

"He bibi wewe naona mwaka huu umeng'ang'ania tu kusuka ukili na kutoa mikeka, au ndiyo unataka kumtunza mkwe wetu?" Ilikuwa ni sauti ya mama Gombea ambaye alikuwa amefika hapo bila ya kuonekana na mama Kadili, kabla ya kuisikia sauti.

"Na wewe nawe mama Gombea, hii mikeka mimi mwenzako nauza ndiyo nipate pesa ya mchezo na ninavyokwambia wiki ijayo zamu yangu."

"Ai mwenzangu mimi nilijua ndiyo michango ya harusi ishaanza hivyo."

Mama Kadili alijua yale maneno anayosema shoga yake, basi kuna kitu anataka kusema. Na hiyo inatokana na tabia yake ya umbea mtaani hapo.

"Basi ndiyo ushapata jambo lako huko, unataka kunitupia hapa, haya lete hicho ulichokileta." mama Kadili.

Mama Gombea aliamua kujibana hapo hapo kwenye mkeka wa mwenzake.

"Kwanza yupo?"

"Nani?"

"Kadili."

"Hayupo."

"Siku ile si nilikwambia kama mwanao ana msichana, tena wa kitajiri."

"Nakumbuka na nikakwambia ndiyo maana siku hizi amebadika kama hana raha vile."

"Basi kumbe huyo msichana amempata kwenye disco huko wanakokwenda, ni kweli yupo anaitwa Edina na anakaa Masaki."

"Wewe mama Gombea hizi habari huwa unazipata wapi?"

"Mimi si ndiyo mbea wenu wa mtaa, sasa unashangaa nini?" Naye aliuliza.

"Lakini naona siku hizi Kadili ana furaha siyo kama wiki zile zilizopita."

"Labda mambo yameshakuwa mazuri, kwa hiyo jiandae tu shoga yangu."

"Lakini mbona mwanangu hana sana mambo ya macho juu juu kwa wasichana navyomuona?"

"Alikuwa hajapata dada wee."

"Haya tutayaona, mimi nipo." mama Kadili aliongea kwa sauti ya chini.

*Itaendelea Jumamosi*

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI


## GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR LOW DENSITY AREA BLOC "C", PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

1152558902

## KUPOTEA KWA CHETI



115286102

**Robert Kombe** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2174/0067** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Nkoma Day. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **4812/2017**

## KUPOTEA KWA CHETI



115288902

**Andrew Makame** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0142-010** kilichotolewa na Baraza la MIthihani la Taifa mwaka 1992 katika shule ya Sekondari Galanos mkoani Tanga. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **PWA/BAG/RB/76584/2019**

## CHETI KIMEPOTEA



115289002

**CHRISTOPHER RUTAJUMULWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.1210/0511** kilichotolewa na DODOMA NURU SEKONDARI mwaka 2004. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/77974/2019.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SOLARKIOSK (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV4** yenye namba za usajili **T 360 DLB.** Chassis namba **ZCA260023334.** Engine namba IZZ0644693. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **991088342856**

115289302

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/06/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 24/06/2019** kampuni ya **GIANT CONTRACTORS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KARATU-ARUSHA** kuelekea **CHUNYA-MBEYA** gari hilo lina namba za usajili: **T 148 CGL na T 296 CLN.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu – mita 17.5**
   **Upana – mita 3.50**
   **Kimo – mita 4.60**
3. Njia itakayotumika KARATU- ARUSHA hadi CHUNYA kupitia DODOMA-IRINGA-MBEYA gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.SC***

215288402


*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223 311*

*Kwa Habari Motomoto usikose*

*Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0767 223 311*



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# SOLSKJAER APEWA FUNGU LA USAJILI MAN U

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekabidhiwa pauni milioni 100 kwa ajili ya kufanya usajili kwenye dirisha hili la kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa chanzo cha ndani cha United, kimeuambia mtandao wa michezo wa ESPN FC kuwa United imetoa kiasi hicho kwa ajili ya usajili kwenye kipindi hiki huku ikitegemea kuuza baadhi ya nyota wake ili kuongeza fedha hizo.

Bajeti hiyo ni sawa na usajili wa mchezaji mmoja wa Juventus, Cristiano Ronaldo aliyetoka Real Madrid kwa dau la pauni milioni 105.

Nyota hao wanaotegemewa kuondoka na huenda wakasaidia usajili huo, ni pamoja na Paul Pogba, Romelu Lukaku na David De Gea ambao wameruhusishwa kutimka.


Hata hivyo, imeshuhudiwa Ander Herrera na Antonio Valencia wakiondoka kama wachezaji huru mwishoni mwa msimu huu, na miezi mitano baadaye kuuzwa kwa Marouane Fellaini kwa dau la pauni milioni 10.5 kwenda Shandong Luneng.

Solskjaer ambaye alikabidhiwa rasmi timu hiyo Machi mwaka huu, akichukua mikoba ya Jose Mourinho baada ya kutimuliwa Desemba, hadi sasa amemsaini aliyekuwa winga wa Swansea City, Daniel James.

United imewaongezea mkataba, Ashley Young, Phil Jones, Chris Smalling na Juan Mata pia kumuongeza beki wa kati wa Leicester na timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, kiungo wa Newcastle United, Sean Longstaff na beki wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka.

Hata hivyo, vijana hao wa United wanatarajiwa kurejea kwa ajili ya msimu mpya wa ligi Julai Mosi, huku wakiwa wametumia pauni milioni 15 hadi sasa.




# MBAPPE APAGAWISHA MASHABIKI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KYLIAN Mbappe amewafanya mashabiki wa Liverpool kuishi na matumaini kwamba pengine mshambuliaji huyo wa Ufaransa anavutiwa na mpango wa kujiunga na timu yao huko Anfield.

Mbappe amekuwa akihusika kwenye matukio mbalimbali yanayoihusisha Liverpool ambayo huenda yakamzindua kocha Jurgen Klopp na kuamua kupeleka ofa ya kutaka huduma ya mshambuliaji huyo.

Ingawa Mbappe hatarajiwi kuondoka Paris Saint-Germain katika dirisha hili la majira ya joto, huku Liverpool nao wakionekana kutokuwa na dhamira ya kutumia fedha nyingi baada ya kuwanasa Alisson na Virgil van Dijk katika madirisha yaliyopita.

Lakini, Mbappe ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia hivi karibuni alionekana akiwa na nyota wa mpira wa kikapu wa Marekani, LeBron James, ambaye ni shabiki mkubwa wa Liverpool, huku kwenye video yao wakiwa pamoja, kofia yenye nembo ya Liverpool ilikuwa ikionyeshwa.

Mashabiki wa Liverpool wamepata mzuka zaidi baada ya kumwona nyota huyo wa PSG akianza kuwafuatilia nyota wa zamani na wasasa wa kikosi hicho cha Anfield kwenye mtandao wa Instagram.

Mbappe aliwahi kuhojiwa hivi karibuni na mtangazaji wa ESPN, Mauricio Pedroza alipoulizwa ni timu gani atapenda kuicheza kwenye gemu ya FIFAM, alijibu ni Liverpool.

Alidai kwamba ameichagua timu hiyo kwa sababu imetoka kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akimtaja kocha Klopp kuwa ni bora.

Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi alisema: "Mbappe? Nina hakika kwa asilimia 200 atabaki kwenye kikosi cha PSG msimu ujao."

# Mendy na simulizi zake katika soka

**MADRID, Hispania**

MCHEZAJI mpya wa Real Madrid, Ferland Mendy, amesema kuwa aliambiwa huenda asicheze tena soka baada ya upasuaji aliofanyiwa akiwa na umri wa miaka 15 kumfanya kutembea kwa usaidizi wa kiti cha kutumia magurudumu.

Beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na Real kwa mkataba wa miaka sita kutoka Lyon wiki iliyopita kwa ada ya pauni milioni 47.1.

"Nilikuwa katika kiti cha magurudumu kwa muda na nilihudumia kipindi cha kati ya miezi sita hadi saba nikiwa hospitali nikifanyiwa marekebisho ili niweze kutembea," alisema Mendy.

"Waliniambia kwamba sitaweza kucheza tena. Lakini sasa niko katika Klabu ya Real Madrid."

Miaka miwili iliyopita, Mendy alikuwa bado akiichezea klabu ya daraja la pili ya Le Havre kabla ya kujiunga na Lyon Juni mwaka 2017. Alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa dhidi ya Uruguay Novemba mwaka jana.

"Mwanzo sikuamini," Mendy alisema kuhusu uhamisho wake katika Klabu ya Real Madrid.

"Hii ni klabu kubwa na kuweza kutia saini nao kwangu mimi ni kitu kizuri zaidi. "Nimefurahia na natumai kwamba kila kitu kitakwenda sawa.

Kuwasili kwa Mendy kumefanya gharama ya Real Madrid msimu huu kukaribia pauni milioni 300.

Klabu hiyo tayari imemsainisha mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard kutoka Chelsea kwa dau ambalo linaweza kuwa zaidi ya pauni milioni 150, pamoja na mshambuliaji wa Serbia, Luca Jovic kutoka klabu ya Eintracht Frankfurt kwa dau la pauni milioni 53, pia wameinasa saini ya beki wa Porto, Eder Militao kwa dau la pauni milioni 42.7.

## HABARI MICHEZO




# ATLETICO
## YAMNASA LLORENTE WA REAL

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid inapanga kumsajili kiungo Marcos Llorente baada ya kutangaza kwamba wamekubaliana na wapinzani wao wa jiji moja, Real Madrid.

Llorente atafanyiwa uchunguzi wa afya kabla ya kusaini miaka mitano pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano na anatajwa kuwa na thamani ya euro milioni 40.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 anajiunga na kikosi hicho kuchukua nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Hispania, Rodri, ambaye anatajwa kwamba anakwenda kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City kwa euro milioni 70.

Atletico tayari imemsainisha mkataba beki, Felipe kutoka Porto na wameripotiwa kwamba wanataka kumleta kinda wa Benfica, Joao Felix.

Usajili huo wanaofanya baada ya wachezaji wake wakubwa kujiandaa kuondoka hapo Atletico akiwamo, Diego Godin, Juanfran, Lucas Hernandez na Antoine Griezmann.

Wapinzani wao, Madrid wamekuwa bize kwenye soko la usajili, kwani tayari wameshawasainisha, Eden Hazard, Luka Jovic na Ferland Mendy.

Katika taarifa ya Madrid iliyotolewa Alhamisi kuhusu Llorente ilisema: "Klabu imemtakia kila la heri (Llorente) kwani alikuwa mfano wa tabia kwa wachezaji wengine tangu alipotua hapo mwaka 2008. Real Madrid inamtakia kila la heri katika hatua yake mpya."

Llorente alicheza mechi saba za La Liga msimu uliopita, ingawa alikuwa chaguo la kwanza kwenye kikosi cha Deportivo Alaves msimu wa 2016-17 alipokuwa akicheza kwa mkopo.

## CECH SASA MSHAURI WA UFUNDI CHELSEA

**LONDON, England**

CHELSEA imemteua golikipa wake wa zamani, Petr Cech kuwa mshauri wa ufundi hapo Stamford Bridge.

Cech atachukua majukumu ya Michael Emenalo, ambaye alijiuzulu hapo Chelsea kwenye nafasi hiyo Novemba mwaka 2017 na nafasi yake ilikuwa wazi.

Chelsea ilisema katika taarifa yake ya Ijumaa: "Kazi yake itakuwa ni kutoa ushauri kuhusu kiwango cha klabu na mambo yote ya kiufundi kwa timu zetu zote."

Mazungumzo ya kumchukua Cech kurudi Stamford Bridge yalianza miezi kadhaa iliyopita kabla ya kucheza mechi yake ya mwisho akiwa Arsenal, ambapo walifungwa 4-1 na Chelsea kwenye fainali ya Kombe la Europa mjini Baku mwezi uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Czech mara baada ya kukabidhiwa mikoba hiyo alisema: "Najihisi kupewa upendeleo na nafasi ya kujiunga na Chelsea FC kwa mara nyingine na kuisaidia kufikia katika malengo mengine.

"Nimekuwa na klabu hii kwa kipindi cha miaka 15 iliyopita. Kwa sasa nimerudi kwenye changamoto mpya na naamini nitakuwa na nafasi ya kuisaidia timu hii kuweza kupata mafanikio zaidi kwa siku za usoni."

Cech ameshinda mataji 13 kwa kipindi cha miaka 11 hapo Chelsea, yakiwamo manne ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2012.

Anaishi jirani na uwanja wa mazoezi wa klabu hiyo wa Cobham na amekuwa na mahusiano mazuri zaidi na mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovich.

# Cameroon kuivaa England 16-bora Kombe la Dunia

**PARIS, Ufaransa**

AJARA Nchout (pichani), alifunga mara mbili, likiwamo bao la dakika za majeruhi na la ushindi kuiwezesha Cameroon kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya New Zealand na kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia la Wanawake.

Cameroon sasa itaivaa England kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 katika michuano hiyo inayoendelea nchini Ufaransa.

Nchout alifunga bao la ushindi dakika ya 95 na kuwawezesha Cameroon kupata ushindi huo.

Cameroon walionekana kuyaaga mashindano hayo wakati Aurelle Awona alipojifunga zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumaliza na matokeo yakawa 1-1.

Nchout alianza kuipa bao la uongozi Cameroon katika kipindi cha pili kwa bao lake 'tamu' la shuti kali.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TORRES: SOKA SASA BASI

Baada ya miaka 18, muda umefika wa kupumzika soka, Jumapili ijayo, Juni 23 saa 4:00 asubuh nitakuwa...

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Atletico Madrid na Hispania, Fernando Torres, ametangaza sasa anatundika daluga baada ya kuwa dimbani kwa kipindi cha miaka 18.

Torres, 35, amekuwa akicheza soka Ligi Kuu ya Japan katika Klabu ya Sagan Tosu, lakini atakumbukwa zaidi kwa kipindi chake akiwa Atletico na Liverpool, pamoja na mafanikio yake akichezea timu ya Taifa ya Hispania.

Torres aliisaidia Hispania kutwaa Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza mwaka 2010, 'La Roja' hao wakitwaa mfululizo ubingwa wa Ulaya, na sasa straika huyo ametangaza kustaafu kupitia mtandao wa kijamii.

"Nina kitu muhimu sana cha kutangaza," aliandika katika akaunti yake ya mtandao wa Twitter. "Baada ya miaka 18, muda umefika wa kupumzika soka.

"Jumapili ijayo, Juni 23 saa 4:00 asubuhi kwa saa za Japan, nitakuwa na mkutano na waandishi wa habari jijini Tokyo kuelezea kila kitu. Tuonane pale."

Torres aliyechomoza kisoka akiwa Atletico, alijiunga nayo mwaka 1995 akiwa na miaka 11, na alipotimiza miaka 17, tayari alikuwa amejumuishwa katika kikosi cha kwanza.

Ingawa msimu wake wa kwanza ulikuwa si wakushangaza, alifunga mara sita katika mechi 36 za 'Segunda', na Atletico ilimpandisha daraja na Torres kuanza kuonja ladha ya La Liga msimu wa 2002/03.

Mabao 13 katika mechi 29 yalifuata na kisha Torres kuendelea kujitangaza mwenyewe katika ligi kama mshambuliaji bora.

Mwaka 2007, aliweka rekodi Liverpool kwa kuwa mshambuliaji ghali zaidi akiripotiwa kugharimu pauni milioni 20, wakati pia uhamisho huo ukimhusisha Luis Garcia aliyehamia upande wa pili, na alionyesha uwezo mkubwa akiwa na 'Wekundu' hao akiifungia mabao 24 katika msimu wake wa kwanza Premier League.

Aliendelea kuwa tishio katika msimu uliofuata licha ya mara kadhaa kuandamwa na majeraha, akifunga mabao 32 katika mechi 46, lakini msimu wa 2010-11, alihitaji changamoto mpya kwa kuhamia Chelsea kwa uhamisho wa pauni milioni 50, na akifanikiwa kubeba Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na 'The Blues' hao.

Lakini bahati ya kiwango na kukumbwa na majeraha mara kadhaa kulimwandama Torres na maisha yake kisoka hapo Stamford Bridge na alipohamia AC Milan yakawa si mazuri, kabla ya kurejea Atletico mwaka 2015.

Mwanzoni mwa miezi 18 yake ya mkopo, Torres alishindwa kurejea katika kiwango chake bora akiwa Atletico, ingawa aliisaidia kushinda Kombe la Europa League mwaka 2018 muda mfupi kabla ya kuondoka kwenda Japan.

## KWA UFUPI

### NEYMAR APIGANIA KURUDI BARCA
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, 27, anaendelea kupigania kurejea Barcelona na hataki tena kuichezea Paris St-Germain. ***(Sport - in Spanish)***

### FELIX AKARIBIA MAN UNITED
Atletico Madrid inakaribia kukamilisha kuinasa saini ya mshambuliaji wa Benfica, Joao Felix, kwa pauni milioni 106.7, hiyo ikiwa na maana Manchester United itamkosa nyota huyo wa kimataifa wa Ureno. ***(Evening Standard)***

### CITY KUIPIKU UNITED KWA MAGUIRE
Manchester City inajiandaa kuipiku Manchester United katika kuinasa saini ya beki wa Leicester City, Harry Maguire, 26, kwa pauni milioni 65. ***(Star)***

### SPURS YAMFUKUZIA FERNANDES
Tottenham imefanya mazungumzo na wakala wa kiungo Mreno Bruno Fernandes, 24, huhusu uwezekano wa kuipata saini yake kutoka Sporting Lisbon. ***(Telegraph)***

### RABIOT ANUKIA KUTUA JUVE
Juventus inatumai kukamilisha dili la kuipata saini ya Adrien Rabiot kutoka Paris St-Germain, wakati huu kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24, akiwa nje ya mkataba majira haya ya joto. ***(Goal)***

### RODRI AITAKA CITY AKIIKATAA BAYERN
KIUNGO wa Atletico Madrid, Rodri, 22, amechagua kujiunga na Manchester City badala ya Bayern Munich, na anatarajiwa kuwagharimu mabingwa hao wa Premier League pauni milioni 62. ***(Kicker - in German)***

### MADRID YAMKOMALIA NEYMAR
Real Madrid imetoa ofa ya pauni milioni 115.5 kwa PSG ili kuipata saini ya Neymar, ikiwa ni pamoja na kuipata huduma ya straika wa Wales, Gareth Bale, 29, ama kiungo Mcolombia James Rodriguez, 27. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### BARCA KUMBAKISHA DEMBELE
RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amerudia nia yake ya kutamani kumbakisha straika Mfaransa Ousmane Dembele, 22, hapo Nou Camp, licha ya Liverpool kumtaka. (Mirror)

### SOLSKJAER, MADDISON KUKUTANA
KIUNGO wa Leicester City, James Maddison, 22, ameomba kukutana na kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye yupo tayari kumhamishia nyota huyo wa kikosi cha England U-21 hapo Old Trafford. ***(Star)***

### FIRPO KUMRITHI MORENO LIVER
Liverpool inataka kuifuata saini ya beki wa kushoto wa Real Betis, Junior Firpo, 22, kama mbadala wa Mhispania mwenzake Alberto Moreno, 26. ***(Mirror)***

### SARRI KUMGEUKIA PJANIC
KIUNGO wa Chelsea na Italia, Jorginho, 27, hatajiunga na kocha wake wa zamani, Maurizio Sarri katika kikosi cha Juventus, na nyota wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina, Miralem Pjanic, 29, anatarajiwa kuwa mbadala. ***(Mail)***

### ZOUMA ATAKIWA JUMLA EVERTON
Everton imefungua meza ya mazungumzo na Chelsea kuhusu uwezekano wa kuipata jumla huduma ya beki Kurt Zouma baada ya Mfaransa huyo kuichezea kwa mkopo msimu mzima uliopita. ***(Telegraph)***

### MAN CITY YAMTAKA RIESGO
Manchester City huenda ikamsainisha mlinda mlango wa Eibar, Asier Riesgo, 35, kwa uhamisho huru na kumfanya Mhispania huyo kuwa kipa wao namba tatu. ***(Manchester Evening News)***

# AZAM YAMNASA MVUYEKURE, YAMSAINISHA TENA CHIRWA

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati, Azam FC wamekamilisha usajili wa kiungo mshambuliaji Mrundi Emmanuel Mvuyekure, kwa mkataba wa mwaka mmoja akitokea KMC, huku pia wakimpa mkataba wa mwaka mmoja zaidi straika wao, Mzambia Obrey Chirwa.

Mvuyekure anayemudu nafasi zote za ushambuliaji, anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Azam FC kuelekea msimu ujao baada ya ule wa kwanza wa winga Idd Selemani 'Nado'.

Nyota huyo alimaliza msimu uliopita akiifungia KMC mabao 10 wakati ikimaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Mvuyekure ambaye pia aliwahi kuicheza Mbao FC, ameshatua nchini tangu jana alfajiri na jana alianza rasmi mazoezi na kikosi hicho kinachojiandaa na michuano ya Kombe la Kagame.

Katika hatua nyingine, Azam FC imemwongezea Chirwa mkataba wa mwaka mmoja, huku kiungo mzawa, Salmin Hoza naye akiongezewa miaka miwili ya kuitumikia klabu hiyo.

Kocha Mkuu mpya wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, ndiye aliyependekeza usajili wa nyota huyo, ambapo hadi sasa katika mapendekzo ya usajili wa nyota wapya wanne, amebakisha nafasi mbili, mmoja akiwa wa ndani na mwingine wa nje.



Mshambuliaji Mzambia Obrey Chirwa akitia saini mkataba mpya wa mwaka mmoja kuendelea kuitumikia Azam FC jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Katwila ataka mapro wengi waruhusiwe Ligi Kuu Bara

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI hoja ya idadi ya wachezaji wangapi wa kigeni waruhusiwe kusajiliwa na kuanza katika kikosi cha kwanza katika msimu ujao ikiwa inaendelea kujadiliwa, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kwake haoni kama kutumia nyota wengi kutaua vipaji vya Watanzania.

Akizungumza na gazeti hili wiki hii, Katwila, alisema wageni wanapokuwa wengi, wanasaidia kuwafanya wachezaji wazawa kujituma kwa sababu hakuna nafasi ya upendeleo katika kikosi cha kwanza.

Katwila alisema endapo, wageni wataanza kuwekewa "vigingi" baada ya kusajiliwa, uamuzi huu ndio utachangia kushusha viwango vya wachezaji wa Kitanzania.

"Kikubwa ni kupambana, mchezaji anapojua anatakiwa kupambana na mgeni, anaongeza juhudi, kuna wageni kadhaa tumeshuhudia wanasugua benchi, hapa tuwaandae wachezaji wetu na mengine yatajibiwa kwa vitendo uwanjani," alisema Katwila.

Kocha huyo aliongeza kuwa serikali pamoja na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanatakiwa kudhibiti wachezaji "wabovu" na hapo ndipo watasaidia kuboresha wachezaji wazawa, ambao watapata nafasi nyingi za kucheza.

"Hata tukijadili sana kuhusu wachezaji wageni, bado uhalisia wanachukua sehemu ndogo katika wachezaji wanaosajiliwa katika Ligi Kuu, asilimia 80 tunatumia wachezaji wa hapa nyumbani, na shughuli zao mnaziona," Katwila aliongeza.

Mtibwa Sugar ambayo msimu wa 2017/18 walitwaa ubingwa wa Kombe la FA na kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka huu, msimu uliopita wamemaliza katika nafasi ya tano, nyuma ya mabingwa Simba, Yanga, Azam FC na KMC FC.

## KMC kambini vita vya Kagame Cup

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya KMC FC inatarajia kuingia kambini keshokutwa Jumatatu kuanza kujiandaa na michuano ya Kombe la Kagame inayotarajiwa kuanza Julai 7-21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

Akizungumza na Nipashe jana, msemaji wa KMC FC, Anuari Binde alisema licha ya kuwa wageni katika mashindano hayo, watakwenda kushindana na si kushiriki.

"Jumatatu tutaingia kambini na kuanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya Kagame," alisema Anuari.

Anuari alisema tayari wamewasiliana na wachezaji wao waliopo mikoani kurudi kujiunga na kambi mapema hasa kutokana na kuyapa umuhimu mkubwa mashindano hayo.

## Waziri Z'bar apongeza mastaa kuifuata Stars

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, amelipongeza Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), pamoja na Taasisi ya Mimi na Wewe kwa kuwasafirisha wachezaji wa zamani wawili kwenda kuishangilia timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 inayoanza kutimua vumbi leo nchini Misri.

Wachezaji wawili waliokwenda nchini Misri ni Said Ibrahimu Njunju na Othman Abdalla 'Fome' ambao waliwahi kutamba miaka ya nyuma katika klabu zao za Malindi na Ujamaa na kuwahi kuchezea timu ya Taifa ya Zanzibar na hata Taifa Stars.

Waziri huyo alitoa pongezi hizo juzi usiku katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume wakati akiwaaga wachezaji hao waliokwenda Misri kwa ufadhili wa Taasisi ya Mimi na Wewe ambayo imegharamia asilimia 100 safari hiyo.

Alisema wachezaji wa zamani wapo wengi, hivyo ni vyema kukumbukwa kupitia harakati zao za soka walizofanya miaka ya nyuma na kwa kuwa walifanikiwa kwa kiasi kikubwa kulitangaza soka la Zanzibar ndani na nje.

Waziri huyo alisema wizara inathamini kwa kiasi kikubwa mchango wa wachezaji hao na kuwataka kushirikiana na Watanzania waliopo Misri katika kuipa hamasa Taifa Sars ili iweze kufanya vizuri zaidi kwani uwezo wanao.

"Mimi ninaimani kuwa timu itafanya vizuri hatakama hatutokuwa mabingwa, lakini tutafikia nafasi nzuri, hivyo mkaipe hamasa... nyie mnaenda huko mnatuwakilisha sisi tuliopo nyumbani ambao tutafuatilia kupitia vyombo vya habari," alisema.

Michezo
Jumamosi Juni 22, 2019
Nipashe



## Torres: Soka sasa basi

HABARI UK 30

ZAMU YA MBRAZIL...



Mshambuliaji Mbrazil Wilker da Silva (kulia) akitia saini mkataba wa kujiunga na Simba jijini Dar es Salaam jana akiwa na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Swedi Nkwabi. **PICHA: SIMBA**

# DA SILVA WA BRAZIL ATIA SAINI MIWILI SIMBA

Ni straika mrefu mwenye nguvu aliyetua akitokea Klabu ya Bragantino, wengine wasubiri...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya juzi kumtangaza kiungo mkabaji, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman kutoka Klabu ya Al Hilal ya Sudan kupitia ukurasa wao wa Instagram, mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba wameendelea na mchakato wa kujiimarisha kuelekea msimu mpya kwa kufanikiwa kuinasa saini ya straika Mbrazil Wilker Henrique da Silva.

Da Silva ambaye jana amesaini mkataba wa miaka miwili wa kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, ametua Simba akitokea Klabu ya Bragantino inayoongoza msimamo wa Serie B nchini Brazil inayoshirikisha timu 20.

Da Silva mwenye umri wa miaka 23, kama bado ana makali kama anavyoonekana katika mikanda yake ya video ambayo Nipashe iliifuatilia jana, ni wazi Simba itakuwa imelamba dume.

Ni mshambuliaji aliyekwenda juu na aliyejengeka vema kisoka, huku akionekana kutumia nguvu zake vizuri dimbani akimudu kukokota mpira na kuwachambua mabeki, lakini pia akiwa na uwezo wa kufunga kwa mashuti ya mbali, hivyo anaonekana anaweza kutengeneza 'kombinesheni' nzuri pamoja na washambuliaji wa Simba, John Bocco na Meddie Kagere.

**Kama ilivyo kawaida ya Simba, katika ukurasa rasmi wa Instagram, picha za Da Silva akisaini mkataba akiwa na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Swedi Nkwabi, zilitapakaa mtandaoni jana.**

Kwa usajili huo, Da Silva anakuwa mchezaji wa nne kusaini rasmi kuichezea Simba baada ya kipa Beno Kakolanya kutoka Yanga, beki wa kati Kennedy Juma kutoka Singida United wote wazawa na Msudan Shiboub.

Da Silva amekuwa mchezaji wa Bragantino tangu mwaka 2015 alipojiunga nayo akitokea Ponte Preta, huku mwaka 2018 akitoka kwenda kuichezea Uniao Barbarense iliyokuwa Daraja la Tatu kabla ya kurejea timu yake hiyo hadi sasa anatua kwa Wekundu wa Msimbazi hao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa zaidi ambazo Nipashe imezipata jana zinaeleza kuwa Simba ipo kwenye mazungumzo na mawakala wa wachezaji kadhaa na wengine wameripotiwa wapo njiani kutua nchini.

Lakini pia taarifa zaidi zikieleza kuwa tayari beki wa kati Mbrazil Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya India na mshambuliaji Ryan Moon kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini wako nchini na mazungumzo yameshafanyika, hivyo ni muda tu unasubiriwa kabla ya kuwatambulisha rasmi.

## Samatta: Ni vita dhidi ya Senegal

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kesho timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' ikitarajiwa kurusha karata yake ya kwanza dhidi ya Senegal kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri, nahodha wa kikosi hicho, Mbwana Samatta amesema amejipanga vizuri kukutana na miamba hiyo katika mchezo wao huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu kwa kila upande.

Tanzania ambayo hii ni mara ya kwanza kushiriki fainali hizo tangu 1980, mbali na Senegal katika Kundi lao la C, pia linajumuisha Algeria na Kenya, 'Harambee Stars'.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya barua pepe kutoka jijini Cairo, Samatta alisema licha ya Senegal kuwa na nyota wengi wazuri atajituma akishirikiana na wachezaji wenzake waanze ili kuhakikisha wanaanza vizuri michuano hiyo.

Samatta alisema, michezo ya kirafiki waliyocheza imewasaidia kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kuanza kuzoea mazingira ya mchezo wanaokwenda kuucheza kesho.

"Kiujumla kila mchezaji morali iko juu, naomba wachezaji tushirikiane ili tutimize lengo letu na kuweza kupata mafanikio tunayoyahitaji tuzidi ili kusonga mbele," alisema Samatta.

Nahodha huyo aliendelea kusema Senegal ni timu bora Afrika ambayo ina kiwango cha hali ya juu, na kusisitiza wachezaji wenzake wacheze kwa kujituma na ushirikiano wa hali ya juu ili kuweza kupata matokeo.

"Siku zote ukijiamini utafanya vizuri, naomba sisi kama wachezaji tujitume kwani mwalimu ameshafanya kazi yake kilichobaki ni juhudi tu," alisema nahodha huyo.

Baada ya mchezo wa kesho, Juni 27 Taifa Stars itashuka dimbani tena kuivaa Harambee Stars kabla ya Julai Mosi, mwaka huu kuhitimisha mechi za hatua ya makundi kwa kuvaana na Algeria.

Katika mechi mbili za kirafiki Stars ilizocheza na timu zilizofungua michuano hiyo ya Afcon jana, ilianza kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya wenyeji, Misri na kisha kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Zimbabwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >